SUPA JACKPOT
TZS. 1,112,462,859
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mtaala** mpya waja na agizo mwalimu wa msingi sharti awe na diploma

UKURASA 2


ama
ALHAMISI MEI 11, 2023
AFYA NA MAZINGIRA
RC ashika bango dai la ushoga mkoani, vikao madiwani kashfa zawasha moto
Mwakilishi UNFPA: Kinga vifo vya wajawazito, 'vichanga' ni wakunga
Wadau Taasisi Moyo waanika ushindi kitaaluma, zao aliloweka Rais Samia
• Ujuzi kufika kila mkoa; ubia na Zambia, Rwanda...

UKURASA 11

# Nipashe


Alhamisi Mei 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581307

www.ippmedia.com

The Guardian nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# Hatimaye familia mwanafunzi wa UDOM yafunguka

• **Yadai** mwili ulivikwa nguo ya kiume; Tume Haki za Binadamu kuchunguza kifo... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**WAZIRI AWESSO ATAJA MAPINDUZI 18 SEKTA MAJI**
WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, mafanikio 18 yamepatikana katika sekta...



UKURASA WA 24
**YANGA YAINGIZA MGUU MMOJA FAINALI CAF**
MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, wameingiza mguu mmoja kwenye...

## Daktari bingwa aibua utata wa ripoti tiba India

UKURASA 5



Aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Balozi Simon Sirro, akipunga mkono wakati wa hafla ya kuagwa baada ya kustaafu utumishi wa jeshi hilo, iliyofanyika Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini, Dar es Salaam jana. **PICHA: RESTUTA JAMES**



## Sirro: Wasiojulikana, mauaji Kibiti yalinitesa

UKURASA 3

**MIILI YA WATU WATANO YAOPOLEWA PORINI** UK.5

**KATUNI** UK.6

# Mtaala mpya: Mwalimu msingi sharti diploma

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

UTEKELEZAJI wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na mitaala ya elimu toleo la 2023 utaanza kwa awamu mwakani, huku walimu watakaofundisha shule ya msingi wakipaswa kuwa na stashahada ya ualimu.

Akiwasilisha rasimu za sera na mitaala hiyo kwenye semina ya wabunge jijini hapo, Kamishna wa Elimu Tanzania, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema katika mapendekezo ya rasimu hizo, walimu watakaofundisha elimu ya msingi itakuwa lazima wawe na stashahada ya ualimu baada ya kumaliza kidato cha sita.

Alisema kwa watakaofundisha elimu ya sekondari, ni lazima wawe na shahada ya ualimu, hivyo walimu waliopo kazini ambao hawatokuwa na sifa hawataondolewa kwenye ajira bali watapewa fursa ya kujiendeleza ili kufikia viwango.

Akitoa ufafanuzi kwa wabunge, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema hakutokuwa na mtihani wa kumaliza elimu ya msingi badala yake kutakuwa na mtihani wa upimaji, ili kuendelea na elimu ya sekondari ngazi ya chini.

"Wanafunzi wote watakaomaliza darasa la saba mwaka 2024 watajiunga kidato cha kwanza Januari 2025 baada ya kufanya mtihani wa upimaji badala ya ule wa kumaliza elimu ya msingi. Kwa mwakani utekelezaji utaanza kwa darasa la awali, darasa la kwanza, darasa la tatu, kidato cha kwanza na kidato cha tano," alisema.

Prof. Mkenda alisema madarasa mengine yote yataendelea na mitaala ya zamani. Lengo ni kuwa na mageuzi ya hatua kwa hatua. Siyo ya haraka.

"Kwa wanafunzi watakaomaliza darasa la saba mwakani, wote wataanza elimu ya sekondari baada ya kufanya mitihani ya upimaji. Hii itakuwa ni hatua ya kutekeleza sera mpya ambayo inaelekeza kuwa elimu ya lazima kwa mtoto wa Tanzania ni kusoma kwa miaka 10 mfululizo ikiwa ni miaka sita ya elimu ya msingi na miaka minne ya sekondari," alisema.

Pamoja na hayo, alisema serikali inakwenda kurudisha katika hadhi yake shule zote za ufundi ambazo zitafundisha mkondo wa amali.

Baadhi ya wabunge wakichangia wakati wa semina hiyo, akiwamo wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage, walishauri serikali kutoa fursa ya kujiendeleza kwa walimu walioko kazini watakaokuwa hawana sifa hizo pendekezwa.

# Familia mwanafunzi wa UDOM yafunguka

**Na Waandishi Wetu**



FAMILIA ya marehemu Nusura Hassan Abdallah, aliyekuwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), imefunguka ikisema taarifa za kifo cha mtoto wao walizipata kutoka kwa mchumba wake, Juma Kundiya ambaye ni mwalimu wa sekondari iliyoko Marangu mkoani Kilimanjaro.

Wakati familia ikisema hivyo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), imeazimia kufanya uchunguzi huru kwa madhumuni ya kubaini ukweli kuhusu tukio hilo.

Uamuzi huo umekuja baada ya kuwapo taarifa kwenye mitandao ya kijamii zikihusisha kifo cha mwanafunzi huyo na ajali aliyopata Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange.

Familia ya marehemu imesema kuhusisha kifo cha mtoto wao Nusura na ajali ya kiongozi huyo wa serikali siyo sawa kwa kuwa mara ya mwisho waliongea naye (Nusura) Aprili 29, 2023 akiwa hai wakati ajali ya Waziri ilitokea Aprili 26, 2023.

Baba, mama mzazi na dada wa marehemu walitoa ufafanuzi huo jana walipozungumza na waandishi wa habari nyumbani kwao eneo la Uwanja wa Ndege, Kata ya Mandewa, Manispaa ya Singida.

Baba mzazi wa marehemu Nusura, Hassan Abdallah, alisema mtoto wao mara ya mwisho aliongeza na mama yake mzazi Aprili 29 japo hawakujua kama alikuwa chuoni au mahali kwingineko.

Abdallah alisema taarifa za kifo cha Nusura alizipata kutoka kwa mchumba wake aitwaye, Juma Kundiya, ambaye ni mwalimu wa sekondari katika shule moja iliyoko Marangu mkoani Kilimanjaro.

"Nilimpigia yule kijana, yaani mpenzi wa Nusura. Akaniambia 'ni kweli alikuja kwangu, lakini alipata homa ghafla. Nikampeleka hospitalini, bahati mbaya akawa amefariki'," alisema.

Abdallah alisema mpenzi wake huyo alidai tukio la kuugua na kufariki dunia likitokea Jumatatu na siku waliyompigia simu ilikuwa Jumatano na alipoulizwa sababu za kutokutoa taarifa kuwa mwenzake anaumwa au amefikwa na umauti, alijibu kuwa alikuwa na mfadhaiko, hivyo alishindwa kutoa taarifa.

"Kijana wakati ninaongea naye, nilimuuliza nini zaidi kilichosababisha kifo cha Nusura, alijibu kuwa sukari ilipanda na baadaye akaniambia kama ameshafariki, aniletee mwili wa mwanangu, ili niuzike na mambo mengine yataendelea," alisema.

Mama mzazi wa Nusura, Amina Shaban, alisema wakati anamtafuta katika simu mtoto wake bila mafanikio, wanafunzi wenzake walimweleza kuwa alikwenda kwa mpenzi wake Moshi, lakini walishindwa kumweleza kilichotokea akiwa huko kutokana na kuogopa.

Alisema kuwa kabla ya umauti kumkuta, mpenzi wa Nusura alituma ujumbe mfupi wa maneno katika simu ya marehemu akimlazimisha aende Moshi wakaonane.

"SMS alizotuma huyo kijana wakati Nusura akiwa bado yupo Dodoma akimlazimisha aende Moshi wakaonane, bahati nzuri hakuzisoma pekee yake bali alimpa na rafiki yake wa chuoni wakazisoma wote," alisema.

Aliongeza kuwa mara mwisho kuongea na mtoto wake (Nusura) ilikuwa siku ya Jumamosi (Aprili 29, 2023) kumpa taarifa ya msiba wa mamake mdogo uliotokea katika Kijiji cha Misuna.

Amina alisema kuwa ilipofika Jumatatu, hakuna mawasiliano yoyote yaliyokuwapo kati yao ndipo alianza harakati za kumtafuta kupitia kwa wanafunzi wenzake bila mafanikio.

"Baada ya kuona ukimya, Jumatatu nikaanza kumtafuta simu yake ikawa inaita tu bila kupokewa, jioni siku hiyo nikampigia tena nikijua muda huo hatokuwa darasani lakini bado sikumpata," alisema.

Mama mzazi huyo alisema baadaye aliamua kuwasiliana na dada yake mkubwa aliyeko Kijiji cha Koresta wilayani Moshi, kwa kuwa alikuwa na mawasiliano na mchumba wake ili kupata taarifa kama alikwenda huko au la.

Alisema kuwa dada yake huyo aitwaye Asia Shaban alimjibu kuwa alikuwa na Nusura lakini bahati mbaya ameshafariki dunia na hivyo wakapewa taarifa na wakamtuma mtu kutoka Singida kufuatilia kwa undani kifo hicho.

Amina alidai kuwa wanafunzi hao walimweleza kuwa wakati wanamtafuta Nusura, walimpigia simu mchumba wake ambaye aliwajibu vibaya kwamba 'Nusura kanizingua na mimi nimemzingua'.

Dada wa marehemu, Kuluthum Shaban alisema katika hali ya kushangaza mtu waliyemtuma katika hospitali aliyofia Nusura, alikuta mwili umevalishwa kanzu.

Kuluthum alisema wana shaka na uchunguzi unaofanywa na vyombo vya dola. Huenda hautotenda haki kwa sababu familia haishirikishwi chochote hadi sasa.

"Tumeambiwa kuna matapishi ya marehemu ambayo uchunguzi unaendelea na yatapelekwa kwa Mkemia Mkuu kuchunguza, lakini hatuna imani maana hatujaona na hayo mabaki ya chakula kama je ni ya marehemu au la," alieleza.

Alisema kutoshirikishwa kwa familia na vyombo vinavyochunguza suala hilo, kunatoa ishara hata majibu yatakayotolewa hawatokuwa na imani nayo.

Wanafamilia hao pia walisema wanashangaa kuona mchumba wa marehemu ambaye alikuwa na Nusura hajakamatwa. Yuko nje, jambo ambalo linatia shaka kama haki itatendeka.

Mwishoni mwa wiki, Chama cha ACT -Wazalendo kiliitaka serikali kuunda tume huru ya kuchunguza suala hilo kwa kuwa uchunguzi utakaofanywa na Jeshi la Polisi umeshakuwa na doa kutokana na kile kilichokiita ushiriki wao kwenye hatua za awali za kuficha ukweli wa taarifa za kifo hiko.

TUME

Taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa THBUB, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu. THBUB inao wajibu wa kuchunguza kifo hicho kwa mujibu wa kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura ya 391.

"Tume inayo mamlaka ya kuanzisha uchunguzi wake yenyewe juu ya malalamiko yanayoashiria uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora pasipo kusubiri kuletewa malalamiko. Kwa muktadha huo Tume imeazimia kufanya uchunguzi wake huru kwa madhumuni ya kubaini ukweli kuhusu matukio hayo," alisema.

Jaji Mwaimu alisema katika kipindi cha takribani wiki mbili, tume hiyo imeona katika vyombo vya habari taarifa ya ajali ya gari iliyomhusu Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Ndugange iliyotokea katika Jiji la Dodoma na kuthibitishwa na Jeshi la Polisi.

"Kwa niaba ya tume, tunapenda kumpa pole Naibu Waziri kutokana na madhara aliyoyapata katika ajali hiyo. Mwenyezi Mungu aendelee kumponya na kumpa afya njema," alisema.

Alibainisha kuwa tume imeona taarifa kupitia vyombo mbalimbali vya habari hususan mitandao ya kijamii kuhusu kifo cha mwanafunzi wa UDOM, Nusura.

"Kwa mujibu wa taarifa imedaiwa kuwa Nusura Hassan Abdallah, alifariki katika Hospitali ya Faraja, huko Himo mkoani Kilimanjaro. Kwa hali yoyote ile taarifa za kifo cha mwanafunzi huyo ni za kusikitisha kwa kuwa kifo hicho, iwe kwa sababu yoyote ile, kimekatisha ndoto ya maisha yake na haki yake ya kupata elimu ya juu.

"Tume inaungana na wazazi wa marehemu, uongozi na jumuiya ya UDOM, ndugu, jamaa na marafiki katika kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe pumziko la amani,"alisema.

Alisema katika siku za hivi karibuni kumekuwapo taarifa katika vyombo hivyo ambazo kwa tafsiri yake zinaonekana kukinzana.

Alisema taarifa hizo zinazokinzana zimekaririwa kutoka katika Jeshi la Polisi, UDOM, Hospitali ya Faraja iliyopo Himo mkoani Kilimanjaro na taarifa za wananchi kupitia mitandao ya kijamii.

***Imeandikwa na Thobias Mwanakatwe (SINGIDA) na Paul Mabeja (DODOMA)***

# Sirro: Watu wasiojulikana, mauaji Kibiti yamenitesa

**Na Restuta James**

MKUU wa Jeshi la Polisi mstaafu, Balozi Simon Sirro (pichani), amesema tukio la kuuawa kwa askari tisa na wahalifu kuchukua silaha zote, mauaji ya watu wenye ualbino na utekaji uliofanywa na watu wasiojulikana ni mambo yaliyomnyima usingizi wakati wa uongozi wake jeshini.

Balozi Sirro aliwaambia waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam wakati wa hafla ya kuagwa kwake kulitumia Jeshi la Polisi iliyofanyika katika Chuo cha Taaluma ya Polisi, Kurasini.

"Yaliniumiza kwa kiasi kikubwa kwa sababu unapokuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, usalama wa raia na mali zao ni jambo la msingi sana. Linapotokea suala kama hilo, IGP huwezi kufurahi... kwa hiyo kinachofanyika ni kutafuta nani amefanya... unaposhindwa kuzuia ni lazima uweke nguvu kuwapata wahusika," alieleza Balozi Sirro.

Alisema kuwa katika baadhi ya matukio walifanikiwa kuwapata wahusika na mengine hawakufanikiwa kuwapata wahalifu.

"Upelelezi unaweza ukafanikiwa na unaweza usifanikiwe. Ninaomba Watanzania waelewe kabisa hilo, siyo kila tukio polisi anaweza kubaini hayo mambo. Kuna mengine tunafanikiwa, mengine hatufanikiwi," alisema.

Balozi Sirro aliongeza "...tukio ambalo siwezi kulisahau ni hili la Kibiti. Askari tisa walipigwa risasi, walikuwa wanatoka kwenye lindo, wakapigwa ambushi kama unakumbuka. Kwa hiyo askari waliuawa, walikuwa ni askari wadogo jeshini, wote tisa, na silaha zote zikachukuliwa."

Alisema askari walifanya kazi kubwa kuwatafuta wahalifu na kufanikiwa kurejesha silaha na kuwaua baadhi ya waliohusika.

"Tuliwapata wahusika na bahati mbaya na wao walishatangulia mbele ya haki. Hili ni tukio ambalo sitolisahau. Ukienda ukakuta askari tisa wote wamepigwa risasi wamelala, siyo jambo dogo," alisema Balozi Sirro, ambaye amelitumikia Jeshi la Polisi kwa miaka 30.

Tukio la kupigwa risasi kwa askari hao lilitokea Aprili 13, 2017 katika Kijiji cha Uchembe, Kata ya Mjawa wilayani Kibiti, Mkoa wa Pwani, baada ya watu waliodaiwa kuwa ni majambazi kushambulia kwa risasi gari la polisi namba PT 3713 Toyota Landcruiser.

Pamoja na mauaji, wahalifu hao waliondoka na silaha za askari hao ambazo ni SMG sita zikiwa na risasi 30 kila moja na long range tatu.

"Kibiti ilikuwa ni shida, ilifika mahala hata viongozi wa kisiasa walikuwa hawaendi pale, lakini nikasema hii ni lazima tupambane nayo," alieleza.

Balozi Sirro alisema wananchi walishirikiana na polisi pamoja na vyombo vingine kudhibiti uhalifu huo na kuomba ushirikiano huo uendelee ili amani idumu nchini.

Kuhusu mauaji ya watu wenye ualbino, alisema ilikuwa ni changamoto kubwa. Polisi wameendelea kukabiliana nayo.

"Tulikuwa tuna changamoto ya panya road (vijana wahalifu wa mitaani) lakini mwisho wa siku tulikwenda vizuri," alisema.



Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi linaendeshwa kwa nidhamu, hivyo inapotokea askari wachache hawazingatii maadili, inahuzunisha na kuchukiza.

"Moja ya jambo ambalo nimemwambia IGP Camilius Wambura, ni kuliangalia hilo sana, kwamba sisi tupo kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania," aliongeza.

Alisema kuwa katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, kulikuwa na uhalifu mkubwa, ambao amesema hivi sasa umepungua.

"Sasa hivi Dar es Salaam maduka yanafunguliwa asubuhi mpaka asubuhi, siyo kazi ndogo," alisema na kufafanua kuwa miaka michache iliyopita, nchi ilikumbwa na matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha ambao ulitishia usalama wa raia na mali zao.

**ASHUKURU WATANZANIA**

Aliwashukuru Watanzania, askari wa ngazi zote na watumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa namna walivyompa ushirikiano akiwa kazini.

Alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumwamini na kumpa nafasi ya kuiwakilisha nchi nchini Zimbabwe, ambako anahudumu kama balozi.

Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camilius Wambura, alisema jeshi hilo linahitaji mabadiliko ya kila mmoja kutokana na wananchi wengi kulilalamikia.

"Nimewaambia watu wangu wote, kila mmoja atake kujua jamii inatuonaje na nini matakwa ya jamii kutoka kwenye jeshi lao?

"Sasa hivi tupo kwenye maboresho ya kuliboresha Jeshi la Polisi kitabia, kiutendaji na mambo mengine mengi. Tunataka tutende kama jeshi lingine la polisi zuri lililopo duniani. Tutende kisasa lakini tutende kiweledi," alisema.

Akimzungumzia Balozi Sirro, IGP Wambura alisema alikuwa mchapakazi mkubwa na hususani kwenye eneo la operesheni, kiasi cha kuteuliwa kuwa mkuu wa idara hiyo.

Hafla ya kuagwa kwa IGP Balozi Sirro, ilihudhuriwa na viongozi wastaafu wa Jeshi la Polisi akiwamo Omary Mahita, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kaspary Mmuya na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Jumanne Sagini, ambaye alikuwa mgeni rasmi.

IGP Wambura alimkabidhi Balozi Sirro kitambulisho cha mstaafu pamoja na gari jipya aina ya Prado Landcruiser VX-L.

Awali, alikagua gwaride maalum lililotoa heshima mbele yake na kuumba umbo la Alfa na Omega; kisha kutolewa nje ya uwanja na gari maalum, kuashiria kuhitimisha utumishi wake ndani ya jeshi hilo.


UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF ENERGY
ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY
(EWURA)

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ROMBO (ROMBO WSSA)

Mnamo tarehe 3 Aprili 2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo (Rombo WSSA). Majedwali Na 1 hadi 3 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Rombo WSSA.

**Jedwali 1: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

| Customer Category | | Current Tariff | Proposed Tariffs | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Domestic | 0-5m³ | 800 | 1,362 | 1,429 | 1,465 |
| | >5m³ | 900 | 1,455 | 1,527 | 1,566 |
| Institutional | | 900 | 1,532 | 1,607 | 1,648 |
| Commercial | | 1,200 | 1,838 | 1,929 | 1,978 |
| Car Wash | | 2,000 | 2,724 | 2,858 | 2,931 |
| Kiosk | | 1,000 | 1,447 | 1,518 | 1,557 |
| Public Schools | | 800 | 1,062 | 1,114 | 1,143 |
| **Weighted Average Tariff** | | **900** | **1,532** | **1,607** | **1,648** |

**Table 2: Current and Proposed Reconnection Fees (TZS/Reconnection)**

| Customer Category | Current Fees | Proposed Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| All customers | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |

**Table 3: Current and Proposed New Connection Fees (TZS/Connection)**

| Customer Category | Current Fees | Proposed Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Domestic | 20% of recoverable expenditures as stipulated in Section 26 of Water Supply Regulations, 2019 | 20% of recoverable expenditures as stipulated in Section 26 of Water Supply Regulations, 2019 | | |
| Institutional | | | | |
| Commercial | | | | |
| Industrial | | | | |

Rombo WSSA imeeleza kuwa bei na ada zinazopendekezwa zitaiwezesha kutekeleza shughuli zilizoainishwa kwenye mpango biashara wake kwa kipindi cha kuanzia 2023/24 hadi 2025/2026 ili kuleta uendelevu wa utoaji huduma za maji. Hasa, kuisaidia mamlaka kurejesha gharama za uendeshaji na matengenezo pamoja na kukidhi gharama za ukarabati, ubadilishaji na uwekezaji mpya na hivyo kutoa maji ya kutosha, safi na salama katika eneo la huduma ya mamlaka, kubadili miundombinu chakavu ya maji, kupanua mtandao wa maji, kununua vitendea kazi na mali nyingine muhimu, kuongeza idadi ya wateja na idadi ya watu inayohudumiwa moja kwa moja na maji.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 18 Mei 2023, katika Ukumbi wa Gosheni uliopo Mkuu, Rombo kuanzia saa 4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la Watumia Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapo juu wakati wowote hadi tarehe 25 Mei 2023. Maelezo zaidi kuhusu maombi ya Rombo WSSA yanaweza kupatikana kwenye ofisi za **Makao Makuu ya EWURA** zinazopatika katika **Jengo la EWURA, 3 Barabara ya EWURA, 41104 Tambukareli, Dodoma au Ofisi za EWURA Kanda ya Kaskazini zilizopo Ghorofa ya Pili, Jengo la PSSSF, Jirani na Kibo Palace Hotel, Arusha Mjini.**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**




Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, Sheikh Dk. Abubakar Zubeir Bin Ally (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa mikopo ya kuwawezesha mahujaji kwenda kwenye ibada za "Hajj na Umrah" inayotolewa na Benki ya CRDB kupitia CRDB Al Barakah Banking, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na wa Kati wa Benki hiyo, Bonaventure Paul (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Idara ya Mashariki ya Kati katika Wizara Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Hemedi Mgaza (kushoto) na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha CRDB Al Barakah Banking, Muhsini Said. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aweso ataja mafanikio 18 sekta ya maji

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, mafanikio 18 yamepatikana katika sekta ya maji, ikiwamo ongezeko la upatikanaji wa majisafi na salama vijijini na mijini.

Amesema kwa wananchi wa vijijini upatikanaji wa huduma hiyo umeimarika kutoka asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asilimia 77 mwaka 2022 na mijini kutoka asilimia 84 mwaka 2020 hadi asilimia 88 mwaka jana.

Waziri Aweso alitoa taarifa hiyo jana bungeni jijini hapo wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alitaja mafanikio hayo ni kukamilika kwa miradi 1,373 ya usambazaji maji na kuanza kutoa huduma kwa wananchi waishio katika vijiji 2,649, hivyo kufikisha vijiji 9,737 vyenye huduma hiyo nchini.

Pia alisema miradi 80 ya usambazaji maji mijini imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi 4,305,801.

Mafanikio mengine, kwa mujibu wa Aweso ni kukwamuliwa kwa miradi 157 na kuanza kutoa huduma kati ya miradi 177 ya vijijini iliyokuwa imekwama kwa muda mrefu.

"Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 218 kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona inayohudumia wananchi wapatao milioni 2.09, kwamba miradi 44 imetekelezwa mijini na miradi 174 vijijini," alisema Aweso.

Lingine ni kuongezeka kwa maabara za ubora wa maji nchini zenye hadhi ya ithibati kutoka maabara moja ya Mwanza iliyokuwapo mwaka 2021 hadi kufikia maabara saba.

Waziri Aweso alisema pia wamefanikiwa kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa maji katika miji 28 yenye thamani ya Sh. trilioni 1.48 baada ya kutiwa saini kwa mikataba ya ujenzi Juni, 2022.

Kwa mujibu wa Aweso, mafanikio mengine ni kuanza ujenzi wa Bwawa la Kidunda linalogharimu Sh. bilioni 329.46 ambalo litawezesha kuwapo kwa uhakika wa maji katika kipindi chote cha mwaka katika Mto Ruvu ambao ni chanzo kikuu cha maji kwa mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani.

"Mafanikio mengine ni kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa 10 ya ukubwa wa kati ya kuvuna maji ya mvua katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji hususani kipindi cha ukame," alisema.

Waziri Aweso pia alisema wamefanikiwa kutoa huduma kwa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka miji ya Tinde na Shelui wenye uwezo wa kunufaisha wananchi 86,980.

"Kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa choteo la maji kwa ajili ya Mkoa wa Kigoma na kuwezesha wananchi wapatao 215,000 kupata huduma ya uhakika ya majisafi na salama," alisema.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni kuanza kutoa huduma kwa mradi wa maji wa Kyaka-Bunazi, Wilaya ya Missenyi-Kagera ambao umewezesha wananchi 75,000 kupata huduma ya majisafi na salama.

Waziri Aweso alisema pia wameweza kutoa huduma kwa mradi wa kusambaza majisafi katika mji wa Orkesumet wilayani Simanjiro unaonufaisha wananchi 52,000 pamoja na mifugo.

Alisema wizara imefanya marekebisho Na.8 ya mwaka 2022 ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 ili kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

Waziri Aweso alisema katika miaka miwili pia wameweza kuimarisha uhifadhi wa vyanzo vya maji nchini, vyanzo 150 vimewekewa mipaka.

Alisema pia Chuo cha Maji kilidahili wanafunzi 2,847, mabweni matano yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 916 yalikarabatiwa, majengo ya madarasa 15 na ofisi 17 yalikarabatiwa na magari matatu yalinunuliwa.

Waziri Aweso alisema mafanikio mengine ni kuimarika kwa matumizi ya mifumo ya TEHAMA ili kuboresha huduma zinazotolewa na sekta ya maji.

# CRDB yazindua mikopo maalum kusaidia mahujaji

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada zake za kupanua wigo wa kuwahudumia wateja, Benki ya CRDB imezindua mikopo maalum ya Hija na Umrah, ikilenga kuwawezesha Waislamu kufikia malengo yao kwa gharama nafuu.

Mikopo hiyo ya Hija na Umrah imekuja kama suluhisho kwa waumini wa dini ya Kiislamu ambao wanataka kufanya safari ya hija lakini wanakabiliwa na changamoto za kifedha. Kupitia mikopo hiyo, Benki ya CRDB inatoa suluhisho rahisi na nafuu, ikiwawezesha wateja kulipia gharama zao za usafiri na malazi.

Uzinduzi wa bidhaa hiyo mpya umekuja wakati mwafaka ambapo Waislamu kutoka sehemu mbalimbali duniani wanajiandaa kutekeleza wajibu wao wa kuhiji. Mwaka huu, Tanzania ina nafasi ya kupata hadi mahujaji 3,000, lakini wengi wao hawana fedha za kutosha kufadhili safari yao.

"Tunafurahi kuja na ubunifu huu wa mikopo Hajj na Umrah kama nyongeza kwenye bidhaa zetu za CRDB Al Barakah Banking. Mikopo hii inathibitisha dhamira yetu ya kutoa ufadhili nafuu za ufadhili kwa wateja wetu wote, hasa wale wanaotaka kutekeleza ibada ya Hijja na Umrah," alisema Bonaventura Paul.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha CRDB Al Barakah Banking, Muhsin Said, alisema mikopo hiyo ya Hajj na Umrah inatolewa kwa masharti nafuu kwa kuwa haihitaji dhamana yoyote, hivyo kutoa fursa kwa waislamu wote nchini kunufaika.

"Mikopo hii inatolewa hadi Sh. milioni 30. Kwa wateja wafanyakazi, benki inafanya uwezeshaji wa hadi asilimia 80 ya gharama zote za safari. Na kwa wafanyabiashara na wajasiriamali, benki inatoa uwezeshaji wa hadi asilimia 50 ya gharama zote za safari," alisema Muhsin.

Katika hafla hiyo ya uzinduzi, Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir, aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuanzisha mikopo hiyo ya ufadhili wa Hija na Umrah, huku akiwahamasisha Waislamu kote nchini kutumia fursa hiyo kutimiza ibada za Hija na Umrah.

"Huu ni mpango mzuri sana kutoka Benki ya CRDB, na ninawapongeza kwa kuja na ubunifu huu. Ninahimiza Waislamu wote wa Tanzania kutumia fursa hii," alisema Sheikh Zubeir huku akiomba Benki ya CRDB kuziwezesha pia taasisi za mahujaji nchini.

Uzinduzi wa mikopo ya ufadhili wa ibada za Hija na Umrah unasisitiza zaidi dhamira ya Benki ya CRDB katika kutoa masuluhisho ya kifedha ya kibunifu na jumuishi kwa wateja wote. Kupata huduma za mikopo hiyo, wateja wanatembelea tawi lolote la Benki ya CRDB.

Benki ya CRDB ilizindua huduma zake za "CRDB Bank Al Barakah," mwaka 2021 ambapo hadi sasa tayari imevutia wateja zaidi ya wateja 30,000 ambao wamenufaika na huduma mbalimbali zinazotolewa zikiwamo akaunti na mikopo.

Ripoti ya Benki hiyo inaonyesha kuwa Benki ya CRDB kupitia Al Barakah Banking imetoa zaidi ya Sh. bilioni 73 kwa wateja tangu kuanzishwa kwake, jambo linaloonyesha ongezeko la mahitaji ya huduma za kibenki zinazofuata msingi ya Kiislamu nchini.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (wa pili kulia), akikabidhi kitendea kazi kwa Justin Minja ambaye ni mmoja wa vijana waliohitimu mafunzo ya VETA kupitia mradi wa KCB 2jiajiri mkoani Kilimanjaro jana. Mradi huo wenye thamani ya Sh bilioni 2.2 umefadhiliwa na KCB Foundation pamoja na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) na kuwanufaisha vijana 960 nchini. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makori na (wa tatu kulia) ni Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa benki ya KCB, Christine Manyenye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miili watu watano yaokotwa misituni

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

WINGU jeusi limetanda wilayani Mbozi katika mkoa wa Songwe baada ya miili ya watu watano wasiofahamika kukutwa imetupwa kwenye msitu wa Mlima Senjele pembezoni mwa Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

Miili hiyo ambayo ni ya wanaume wanaokadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 25 na 30, inadaiwa kutupwa katika eneo hilo usiku wa kuamkia jana na watu wasiojulikana.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi (ACP) Theopista Mallya, alisema miili hiyo ilikutwa jana asubuhi na kuchukuliwa kwenda kuhifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi. Alisema chanzo cha vifo vya watu hao hakijulikani na kwa sasa wanasubiri taarifa ya kitabibu kutoka kwa madaktari ili wajue kiini chake.

"Ni kweli kuna tukio hilo lakini miili hiyo ni ya watu wasiofahamika. Tumeihifadhi katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi na kwa sababu watu wenyewe hawafahamiki, nawaomba wananchi ambao wamepotelewa na ndugu zao waende kuitambua," alisema Kamanda Mallya. Aliwataka wananchi wenye taarifa za tukio hilo kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili wahusika wafahamike na hatua zichukuliwe dhidi yao.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo ambao ni madereva wa malori, waliliomba Jeshi la Polisi kuongeza ulinzi katika eneo hilo kwa kufanya doria za mara kwa mara ili kuzuia matukio kama hayo ambayo yanatisha.

Mmoja wa mashuhuda hao, Damas Thobias, alisema lori analoendesha lilipata tatizo jana jioni jirani na eneo ilipookotwa miili hiyo lakini aliamua kusogea mpaka eneo ambalo askari wa usalama barabarani wanasimama.

Alisema jirani na eneo ilipookotwa miili hiyo, jioni palikuwa na gari aina ya Toyota Canter ambayo ilikuwa imefunikwa turubai lenye rangi ya bluu na lilikuwa kama limeharibika.

Baada ya kupambazuka, alisema alikwenda kumwangalia rafiki yake ambaye naye alikuwa amepata tatizo ndipo wakaona miili hiyo ikiwa imetupwa kwenye korongo.

"Asubuhi wakati natembea nilikutana na mtu mmoja ambaye alikuwa amechafuka mwili mzima una matope na alikuwa hajui anakoelekea. Sikuhangaika naye kwa sababu eneo lenyewe hili ni baya na huwa tunakutana na watu wengi wa ajabu," alisema Damas.

Alisema baada ya kuiona miili hiyo alihisi pengine yule aliyemwona asubuhi alikuwa miongoni mwa walionusurika kwenye tukio hilo na alikuwa anajiokoa.

Dickson Mbuta ambaye ni dereva wa lori, alisema walipoiangalia miili hiyo walibaini kuwa ilikuwa na majeraha ambayo yalikuwa yanatoka damu na kwamba watu hao walikuwa wamevuliwa nguo.

Aliiomba serikali kuongeza ulinzi kwenye eneo hilo kwa maelezo kuwa hali ya usalama siyo nzuri kutokana na kuwa mbali na makazi ya wananchi.

Mbuta alisema askari wa usalama barabarani ambao huwa wanalinda eneo hilo wanatakiwa kuongezewa nguvu ili kuimarisha zaidi ulinzi.

Eneo hilo la Mlima Senjele miaka ya nyuma lilikuwa linakabiliwa na matukio mbalimbali ya uhalifu ikiwamo utekaji hali iliyolifanya Jeshi la Polisi kuweka utaratibu wa kulinda hasa nyakati za usiku.

# Daktari bingwa aibua utata ripoti ya tiba nchini India

**Na Grace Gurisha**

DAKTARI Bingwa wa Upasuaji wa Magonjwa ya Kifua, Shingo na Tumbo, Maurice Mavura, ameichambua ripoti ya Hospitali ya Apollo ya India katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akidai ina upungufu kuonyesha Florence Samwel hana saratani wakati anayo.

Samwel ambaye ni mfanyakazi wa Wizara ya Kilimo, alifungua kesi ya madai mahakamani hapo akidai fidia ya Sh. milioni 500 dhidi ya Hospitali za TMJ na Hindu Mandal za jijini Dar es Salaam pamoja na Dk. Mavula kwa madai kuwa alipewa majibu ya saratani wakati hana ugonjwa huo.

Dk. Mavura alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ramadhani Rugemalira wakati akitoa utetezi wake katika shauri hilo kwa kuwa ndiye aliyemfanyia upasuaji mlalamikaji kwa kuondoa tezi joto (rhyroid gland) za upande wa kulia na kushoto.

Akiongozwa na wakili wake, Ngasa Ganja, Dk. Mavura alidai ripoti hiyo ilikuwa inajumuisha vipimo vya Ultrasound na CT Scan vya mgonjwa ambaye alikwenda India kwa ajili ya matibabu ya mionzi, baada ya kuona atachelewa kupata huduma hiyo katika Taasisi ya Saratani Ocean Road.

Alidai ripoti hiyo inaonyesha alipimwa shingo, kifua na tumbo na inaonekana mtu wa ultrasound si mtaalamu kwa sababu ripoti inaonyesha waliona tezi lipo wakati yeye aliliondoa.

Pia alidai katika ripoti hiyo waliona tezi zingine zimeota pamoja na viuvimbe kwenye mapafu. Pia alidai kuwa waliona kuna dalili za ugonjwa kwenye pingili za shingo.

"Waliona viashilia vya saratani lakini hawakutaka kwenda mbele zaidi kupima hayo mabadiliko. Unapoona uvimbe kwenye mapafu ni lazima upime ili ujue kama ni TB (kifua kikuu) au saratani. Ripoti hii ina changamoto walivyohitimisha na ni kinyume cha walivyoona,"alidai.

Pia alidai katika ripoti hiyo ilionyesha kuwa tezi la kulia ndilo lililopimwa na kuonyesha halina saratani, wakati la upande wa kushoto ndilo lenye saratani, hivyo walitumia kioo cha maabara kama chaguo la watu wa maabara.

Hakimu Rugemalira alitaka Dk. Mavura aieleze mahakama kuhusu hitimisho la ripoti hiyo kama mlalamikaji ana saratani au la na kudai kuwa ilihitimishwa kuwa hana saratani na Februari Mosi, 2018 aliruhusiwa kutoka hospitalini kwa sababu hakuwa na sababu ya kukaa huko.

Wakili wa mlalamikaji, Norbet Mlwale, alimwuliza Dk. Mavura kwanini fomu ya kuridhia kufanyiwa upasuaji iliyotiwa saini na Samwel haionyeshi kiungo gani kitaondolewa?

Dk. Mavura alidai fomu hiyo haionyeshi kwa sababu Samwel alijua ni kiungo gani kinaondolewa kupitia elimu aliyompa kwa njia ya mdomo.

Akijibu swali lingine, Dk. Mavura alidai kuwa baada ya kumfanyia upasuaji, Samwel hakumwonesha mgonjwa wala ndugu yeyote kiungo alichokitoa na baada ya upasuaji mgonjwa alipoamka, tayari kiungo kilikuwa kimeshapelekwa kwenye uchunguzi.

Akijibu swali la wakili wa TMJ, Josephat Mabula, Dk. Mavura alidai kuondolewa kwa tezi la kulia haikujalisha kama limeathirika au la ili matibabu yatimie lazima liondolewe tezi la pili.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu matumizi sahihi ya dawa iendelee kutolewa

**MARA** kwa mara wataalamu wa afya wamekuwa wakisisitiza watu kuacha kuchukua uamuzi wa kumeza dawa au kufanya jambo lolote pindi wanapohisi dalili zisizo za kawaida katika miili yao.

Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba baadhi ya watu wanapojihisi homa au kuwa na dalili za malaria, kwa mfano, hukimbilia kumeza dawa. Hatua hiyo wakati mwingine imekuwa ikisababisha maradhi na madhara mengine yakiwamo kuibuka kwa magonjwa kama saratani au kutengeneza sumu mwilini kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya dawa.

Katika kampeni kama hizo, iko moja inayosisitiza kuwa si kila homa ni malaria hivyo mtu anapojihisi hali tofauti katika mwili wake, asitumie dawa na badala yake aende katika kituo cha kutolea huduma za afya na kufanyiwa vipimo hatimaye kupewa dawa zinazostahili kwa ugonjwa aliobainika kuwa nao.

Licha ya watu hao kuchukua uamuzi huo, wamiliki wa maduka ya dawa au wafanyakazi wao wamekuwa wakielekezwa mara kwa mara kutotoa dawa kwa mtu yeyote bila kuwa na cheti cha daktari au kuwaandikia matibabu kwa kuwa hawana fani ya utabibu.

Pamoja na msisitizo huo, wako watu ambao wameendelea kufanya hivyo kwa kumeza dawa au kwenda kwenye maduka ya dawa na kuwaeleza wauzaji kisha kupewa dawa na kuzimeza. Hali hiyo, kama ambavyo imekuwa ikisisitizwa na wataalamu na viongozi wenye dhamana katika afya, ina athari kubwa kwa wale ambao wamekuwa wakipuuza maelekezo hayo.

Hivi karibuni kwa mfano, mkoani Arusha, mwananchi mmoja ameripotiwa kuwa ameoza vidole vitano vya mkono baada ya kudaiwa kuchomwa sindano katika duka la dawa baada ya kuelezwa kuwa ana maambukizi katika njia ya mkojo (UTI). Ilidaiwa kuwa vidole hivyo vya mkono wa kushoto viliungua kwa kubadilika rangi na kuwa vyeusi muda mfupi baada ya kuchomwa sindano hiyo mkononi.

Baada ya kupatwa na tatizo hilo, mtu huyo alipelekwa katika hospitali ya rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru kwa uchunguzi zaidi na kubainika kuwa vidole hivyo vimeharibika, hivyo anatakiwa kukatwa kwa kuwa vimeoza baada ya damu kushindwa kufika katika eneo hilo kutokana na mishipa inayosambaza damu kuziba.

Wataalamu wa afya katika hospitali hiyo, akiwamo daktari bingwa aliyemfanyia uchunguzi na kutoa uamuzi wa kukatwa vidole hivyo, kama ilivyo ada, walitoa tena angalizo kuwataka watu kuacha kuchukua uamuzi wa kutumia dawa au kupata huduma katika sehemu zisizostahili zikiwamo maduka ya dawa.

Pamoja na ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya juu ya matumizi sahihi ya dawa, jambo hilo limeonekana kama linaingilia upande mmoja wa sikio na kutokea upande wa pili. Kwa maneno mengine, watu hao ambao wamekuwa wakipuuza ushauri huo, wamekuwa kama sikio la kufa ambalo katu halisikii dawa.

Kwa ujumla, kuna athari kubwa katika utumiaji wa dawa bila kufuata ushauri wa kitabibu kutoka kwa madaktari. Miongoni mwa athari hizo ni dawa hizo kutengeneza sumu katika mwili na kusababisha baadhi ya viungo muhimu katika mwili wa binadamu vikiwamo figo, moyo na ini kuharibika. Wakati mwingine, dawa hizo zinapoingia mwilini na kushindwa kutibu ugonjwa usiohusika, mtu anaweza kupata maradhi makubwa kama saratani.

Ni vyema wataalamu wa afya chini ya Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta hiyo, wakatoa elimu zaidi juu ya matumizi sahihi ya dawa ikiwamo kutumia zile ambazo wameandikiwa na madaktari katika vituo vya huduma za afya baada ya kufanyiwa uchunguzi na kubainika kuwa na ugonjwa halisi. Hali hiyo, ni dhahiri kwamba itaepusha matatizo mengi yanayoweza kujitokeza na hatimaye kuwaponyesha maelfu ya Watanzania.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



Na Halfani Chusi

# Hongera serikali kuamua kuwakumbatia wabunifu kupitia vitendo halisi

**JAMBO** jema ni pale mwenye mamlaka anapotamka kauli inayoleta ahueni kwa walio chini yake, na hata uthubutu wa kujali na kuanza kushughulikia yanayowasibu walioko chini yake.

Ndiyo hatua iliyofanywa na Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, anapowaahidi wajasiriamali wabunifu, kwamba serikali ipo kwenye mchakato wa kuwaongezea nguvu ili waweze kukuza biashara zao.

Anawafariji kwamba, kukamilika hatua hiyo kutawafanya wabunifu wajiamini wakitambua serikali inawathamini na kuweza kuuza bidhaa zao nje ya nchi.

Kiongozi huyo aliyetumia kilele cha maadhimisho ya Siku ya Milki Ubunifu Duniani yaliyofanyika Dar es Salaam, na kuratibiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa kushirikiana na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO).

Kwenye maadhimisho hayo, anasema hatua hiyo itawawezesha wajasiriamali wabunifu kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria akisisitiza wataweza kujikwamua zaidi kiuchumi kupitia bidhaa wanazo zalisha.

Anaagiza muhimili wa mahakama, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), BRELA, Ofisi ya Haki Miliki Tanzania (COSOTA), na tume ya ushindani kuhakikisha wanakuwa na majadiliano yenye mikakati ya kutatua vikwazo walivyoviibua wabunifu na wajasiriamali.

Waswahili husema, chanda chema huvikwa pete. Hivyo, kwa kutambua umuhimu wa hoja ya mkuu wake, Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa naye anabainisha kuwa maadhimosho hayo yalilengea kutambua mchango wa miliki bunifu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kuwajengea watu ufahamu juu ya miliki ubunifu hataza, hakimiliki za alama za biashara na huduma.

Anasema maadhimisho hayo yaliyokuwa na kauli mbiu isemayo 'wanawake na miliki bunifu, kuongeza kasi ya ubunifu katika biashara' lengo lake ni kutambua mchango wa wabunifu wanawake katika kukuza biashara na nafasi yao katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Shughuli hizo ni pamoja na mijadala kuhusu miliki ubunifu, ambayo itahusisha sekta za umma na binafsi kwa pamoja watajadili kuhusu mafanikio na vikwazo wanavyokutana navyo kwenye shughuli zao hasa za ubunifu katika kukuza biashara.

Anaeendelea na ufafanuzi kwamba "majadiliano hayo yatawekewa mikakati ya namna bora ya kutatua vikwazo vya wajasiliamari ili kuwawezesha kufanya kazi zao kisheria na kujiamini zaidi katika kukuza bunifu zao"

Matazamo wa kina uinagusa shuhuda zao kwamba, zitakuwa chachu ya kushawishi wabunifu na wajasiliamari wengine kutambua umuhimu wa kutumia miliki bunifu katika kukuza biashara.

Ni hoja zinazoungwa mkono na wajasiliamali wabunifu waliojitokeza kwenye madhimisho hayo, Jack Mbeleli, anayesema kauli ya serikali imerejesha matumaini na kuwaongezea tija kwenye ukubuni wa bidhaa zenye viwango zinazoweza kuleta changamoto ndani na nje ya nchi.

Mbunifu mwingine, Imani Kilamba, anaishukuru serikali kwa kuahidi kuwakumbatia, akinena kuwa hiyo ni hatua nzuri na itachochea maendeleo kwa wajasiliamali na ukuji wa uchumi wetu.

Kwenye maadhimisho hayo, pia wabunifu na wajasiriamali katika nyanja mbalimbali walipewa vyeti vya ushiriki na tuzo kwa waliofanya vizuri na kupata mafanikio kupitia miliki bunifu.

Maadhimisho hayo yalifanyika Aprili 28 baadala ya 26 ili kupisha Sikukuu ya Muungano na yatakuwa yanafanyika kila mwaka.

## TANGAZO

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 2022

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-22 | Mwaka uliopita 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,226 | 4,150 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,183 | 3,760 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 52,469 | 41,308 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 3,298 | 1,119 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 6,498 | 42,364 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 67,768 | 34,677 |
| 12 | Mali Nyingine | 86,871 | 4,146 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 3,061 | 1,203 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **233,374** | **132,727** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 48,123 | 25,469 |
| 18 | Amana za Wateja | 146,554 | 113,060 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 4,436 | 6,644 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,371 | 5,036 |
| 27 | Dhima Nyingine | 6,194 | 3,316 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **207,678** | **153,525** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **25,696** | **24,485** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 5,097 | 487 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (41,136) | (37,540) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,211 | 1,015 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **25,696** | **24,485** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 614,603 | 945,310 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 3,709 | 4,228 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 287 | 579 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.0% | 13.8% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.5% | 5.9% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 44.9% | 59.9% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 29.0% | 40.3% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 54.3% | 76.6% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 26.1% | 5.7% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 31.1% | 3.8% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 13,786 | 12,385 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,454) | (4,053) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **9,012** | **8,291** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (320) | (41) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba :** | **11,478** | **8,855** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,751 | 1,123 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 9,669 | 7,709 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 57 | 23 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(16,840)** | **(15,738)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (7,580) | (6,782) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (1,748) | (1,032) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (7,513) | (7,924) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,650** | **1,409** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (2,439) | (394) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,211** | **1,015** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | | |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,211** | **1,015** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 132 | 128 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.19 | 0.16 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 8 | 7 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.77% | 0.79% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 14.55% | 5.75% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 66.65% | 74.10% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 0.92% | 0.74% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Limbikizo la Mwaka ya sasa 31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-21 |
|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **3,650** | **1,409** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| - Hasara Katika Mali | 1,946 | 1,656 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo iliyoharibika | 320 | 41 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Mabadiliko Halisi ya riba | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| - hasara ya mabadilisho ya mkopo | - | - |
| - Kodi Iliyolipwa | (1,328) | (411) |
| - hasara ya mabadilisho ya mtaji | - | - |
| **II. Mabadiliko ya mtaji wa kazi** | | |
| - Badiliko Halisi Katika amana iliyobakizwa | 960 | (977) |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 3,537 | (15,732) |
| - Badiliko Halisi Katika amana ya serikali | (31,798) | (9,769) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,689) | (1,655) |
| - Badiliko Halisi Katika amana ya bank zingine | - | - |
| - Badiliko Halisi Katika amana ya mteja | 31,285 | 6,451 |
| -Riba iliyopokewa | - | - |
| -Riba iliyolipwa | 106 | 68 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (63,433) | (13,690) |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(56,443)** | **(32,612)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,158) | (1,367) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (42) | (4) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(1,200)** | **(1,371)** |
| ***IV. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (1,315) | (1,248) |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **(1,315)** | **(1,248)** |
| V. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(58,958)** | **(35,230)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka | 24,857 | 60,088 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka | **(34,101)** | **24,857** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (36,526) | 487 | - | - | 24,485 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,211 | - | - | - | 1,211 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | (4,610) | 4,610 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(39,925)** | **5,097** | **-** | **-** | **25,696** |
| **Mwaka uliopita 2021** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,053) | - | - | - | 23,471 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,015 | - | - | - | 1,015 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | (487) | 487 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(36,526)** | **487** | **-** | **-** | **24,485** |

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | |
|---|---|---|---|
| 1 | 1.Gbenga Makinde<br>**Ofisa Mtendaji Mkuu** | *Imesainiwa* | *27th April, 2022* |
| 2 | Benson Msangi<br>**Mkuu wa Fedha** | *Imesainiwa* | *27th April, 2022* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | *Imesainiwa* | *27th April, 2022* |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | |
|---|---|---|---|
| 1 | 1. Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *27th April, 2022* |
| 2 | 2.Ebele Ogbue<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *27th April, 2022* |





United Bank For Africa ( Tanzania ) Limited is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, one of Africa's leading financial institutions offering universal banking to more than 7 million customers across 750 brances in Africa , USA and Europe .

**Africa**
- Tanzania
- Burkina
- Cameroon
- Chad
- Congo Brazzaville
- Congo DRC
- Côte d'ivoire
- Gabon
- Ghana
- Guinea
- Kenya
- Liberia
- Mali
- Mozambique
- Senegal
- Sierra Leone
- Benin
- Uganda
- Zambia

**Europe**
UK
France

**USA**
New York



# Waitara alia tena bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Tarime Vijiji (CCM), Mwita Waitara, kwa mara nyingine ameangua kilio bungeni na kusababisha taharuki kwa madai kuwa hajaridhishwa na majibu ya serikali.

Hii ni mara ya pili kwa mbunge huyo kuangua kilio bungeni. Mara ya kwanza alilia kutokana na mgogoro wa muda mrefu baina ya wananchi wa jimbo lake na Hifadhi ya Taifa Serengeti (SENAPA). Pia mgogoro kati ya wananchi na Mgodi wa Barrick North Mara.

Juzi, mbunge huyo aliangua kilio tena, akizua taharuki ndani ya Ukumbi wa Bunge baada ya kupewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisikitike sana kumbe watu wa Tarime hawajui adui yao mkubwa ni nani... Waziri wa Madini akihitimisha hoja ya bajeti yake hapa alisema malipo ya fidia hayatafikia mwezi wa Juni yatakuwa yamelipwa.

"Maeneo ya Nyamichele mgodi umeniambia mimi kuwa imekwenda kwenye bodi kuomba maombi maalum ili wananchi walipwe. Kwa majibu haya, hili eneo limekaa zaidi ya miaka 11 hawajalipwa fidia. Haya majibu ya leo (jana) ni ya maumivu," alisema.

Alipotakiwa na Mwenyekiti wa Bunge, David Kihenzile, kuuliza swali, Waitara alisema hana swali la kuuliza na kuanza kulia, hali iliyozua taharuki na kuzimiwa kipaza sauti na kutakiwa kufuata utaratibu kama swali lake halijajibiwa.

Katika swali lake la msingi, mbunge huyo alihoji lini wananchi wanaodai fidia katika maeneo ya Mgodi wa Barrick North Mara; Komarera, Nyamichele na Murwambe watalipwa.

Katika majibu ya Wizara ya Madini yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, ilielezwa kuwa mgodi huo ulionyesha nia ya kuchukua baadhi ya maeneo



ya vijiji vya Komarera, Nyamichele na Murwambe ambavyo ni sehemu ya vijiji vinavyozunguka mgodi huo.

"Baada ya wananchi wa vijiji hivyo kupata taarifa ya maeneo yao kuhitajiwa na Mgodi wa Barrick North Mara, walianza kuongeza majengo haraka, maarufu Tegesha. Hali hiyo ilisababisha mgodi huo kuachana na maeneo hayo kwa kuwa hayaathiri uendeshaji wa shughuli zao za kila siku," alisema.

Mbunge wa Rorya (CCM), Jafari Chege, alisimama kuomba mwongozo wa Spika kwa kutumia kanuni ya 76 kwenye swali hilo la Waitara.

Alisema kutokana na mbunge kutoridhika na majibu ya serikali na kusababisha taharuki ndani ya Bunge na haijawahi kutokea, aliomba mwongozo wa kiti ili kuweka sawa jambo hilo.

Akijibu mwongozo huo, Mwenyekiti Kihenzile alisema watapitia hoja ya mbunge huyo na kuangalia yaliyotokea bungeni kama yanaruhusiwa na kiti kitatoa mwongozo.

Nje ya ukumbi wa Bunge, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye alionekana akimtuliza Waitara. Hata hivyo, mbunge huyo alisikika akisema 'ngoja nikapumzike kwanza. Nitarejea'.




Mkurugenzi wa Tehama na Operesheni wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Jema Msuya (wapili kulia), akishirikiana kushika bango na Mkurugenzi Mtendaji wa benki ya Letshego, Omar Msangi (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi wa Letshego, Simon Jengo (wapili kushoto) na Mkuu wa kitengo cha Operesheni, Kolimba Tawa, wakati wa uzinduzi wa muungano wa benki hizo, jijini Dar es Salaam jana, utakaowezesha kuweka pesa kupitia matawi yote pamoja na mawakala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watengenezaji pombe za kienyeji kutambuliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ina mpango wa kuanza mchakato wa kuwatambua watengenezaji wote wa pombe za kienyeji ili kuwaelimisha na kutengeneza kwenye mazingira mazuri, teknolojia na kutumia vifungashio bora.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu maswali ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM),Agnes Hokororo, Hokororo alitaka kujua kwa nini Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) lisijielekeze katika kuboresha pombe za mvuke ya mabibo badala ya kutoa elimu pekee.

Hokororo pia alihoji serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti na kurasimisha pombe kali ya mwiki inayotokana na mabibo ili kuliongezea thamani korosho.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Kigahe alisema serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha teknolojia zinazotumika kuzalisha pombe hizo za kienyeji na kubuni teknolojia rahisi.

Alisema kupitia SIDO wanatambua watengenezaji wote wa pombe hizo ili kuwaelimisha kuhusu mazingira mazuri ya kutengenezea pombe, kuwaelimisha kuhusu teknolojia rahisi kutengenezea pombe hizo na namna kufanya ufungashaji ili kuziboresha zaidi.

"Kutokana na changamoto zinazowakabili wazalishaji wa pombe za kienyeji na kushindwa kukidhi matakwa ya viwango na kukosa ithibati ya ubora, serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na SIDO imeweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wazalishaji hao," alisema.

Hata hivyo, alisema hadi Oktoba, mwaka jana, leseni 43 za ubora zimetolewa kwa bidhaa za pombe za kienyeji na maombi mengine mapya 22 yako kwenye hatua za tathmini kuelekea kupata ithibati ya ubora.

# Wachanga milioni 56/- kuboresha shule

**Na Julieth Mkireri,** VIGWAZWA

HATIMAYE kero ya muda mrefu iliyokuwa inawakabiliwa wanafunzi wa vitongoji vya Kengeni, Migude na Miomboni, Kijiji cha Milo, Kata ya Vigwaza kutembea umbali mrefu kwenda shule imetatuliwa kwa wananchi kujichangisha Sh. milioni 56.7 za ujenzi.

Wanafunzi hao walikuwa wakisoma katika Shule ya Msingi Milo ambayo hadi kuifikia, wanafunzi walilazimika kupita kwenye makorongo na pori hali iliyozua hofu kwa wazazi wao pia.

Kero hiyo imeondolewa baada ya wananchi kuchanga Sh. milioni 56.7 na kufanya ukarabati vyumba vitano vya madarasa na vyoo kisha kuwahamisha wanafunzi shuleni humo.

Katika Shule ya Awali ya Milo, inaelezwa kuwa kipindi cha mvua maji yakijaa kwenye makorongo hayo wanafunzi wanakwama kwenda shule hadi mvua zitakapokoma.

Mkazi wa Kijiji cha Milo, Hamida Adam, ambaye watoto wake walikuwa wanasoma shule hiyo, alisema kitendo cha shule hiyo kuhamishiwa karibu na makazi ya wananchi kitaondoa hofu ya wazazi wanafunzi wanapochelewa kurejea nyumbani.

Ashura Sefu, alisema wananchi wamefurahishwa na kuhamishwa kwa shule hiyo ambayo sasa wanafunzi watasoma sehemu salama na kwa muda wote mvua na kiangazi.

Baadhi ya wanafunzi, Witness Amos na Hemed Mohamed, walisema mvua zikinyesha walikuwa hawaendi shuleni kutokana na mazingira ya njia wanayopita kujaa maji na kushindwa kuhimili kuvuka katika maeneo yenye makorongo.

Akizindua majengo hayo kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chalinze, Ramadhan Possi, aliwahimiza wananchi kutunza majengo hayo ili watoto wasome katika mazingira mazuri.

Alisema halmashauri itatoa fedha kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya darasa moja, nyumba ya walimu na madawati 60 kuondoa vikwazo vilivyoelezwa katika shule hiyo.

Alisema uongozi wa kijiji unatakiwa kuzingatia kusimamia fedha hizo kwa uadilifu na kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

Diwani wa Vigwaza, Mussa Gama, alipongeza jitihada za uongozi wa kijiji kuibua mradi wa ukarabati wa majengo hayo ambao umetatua kero walizokuwa wakikumbana nazo wanafunzi, ikiwa ni pamoja na kukosa masomo kipindi cha mvua.

Gama alimshukuru pia Mbunge Ridhiwani kwa kutoa madawati zaidi ya 40 kwa ajili ya shule hiyo na kuahidi kusimamia utatuzi wa kero nyingine za shule hiyo.



# Miche milioni 12.6 mkonge yasambazwa

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema hadi Aprili, mwaka huu, Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), imesambaza miche milioni 12.6 katika halmashauri 15 nchini.

Alitoa taarifa hiyo jana, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio ya TSB katika kuongeza uzalishaji wa miche ya mkonge.

Waziri Bashe alisema miche hiyo inatosha kupandwa kwenye eneo la hekta 3,158.38 kwa wakulima wadogo walioko halmashauri za Muheza, Korogwe, Handeni, Kilosa, Mkinga, Singida, Tarime, Bunda, Rorya, Mkuranga, Rufiji, Ruangwa, Bariadi, Shinyanga na Same.

Bashe alisema Wizara ya Kilimo, kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Mlingano, Muheza mkoani Tanga, mwaka ujao wa fedha itaanza ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya mkonge kwa njia ya chupa.

"Kuhusu utafiti wa mbegu na kuhakikisha uhifadhi wa mbegu za asili, wizara kupitia TARI Mlingano, imeendelea kutunza vinasaba 60 vya mkonge," alisema Bashe. Bashe pia alisema mwaka 2020/21 tani 36,170 za mkonge zilizalishwa nchini, mwaka 2021/22 (tani 44.151) na mwaka 2022/23 tani 48,262.99.

Alisema hadi kufikia Aprili, 2023, uzalishaji wa singa za mkonge umefikia tani 48,262.99, sawa na asilimia 80.4 ya lengo la kuzalisha tani 60,000.

Waziri huyo pia alisema TSB imetoa mafunzo ya kilimo bora cha mkonge kwa wakulima wadogo 3,952 na wakulima wakubwa 17 ikilinganishwa na lengo la kuwafikia wakulima 8,000.

Hadi sasa, alisema TSB imewaunganisha wakulima 2,500 na soko kwa mfumo wa zabuni ikilinganishwa na lengo la wakulima 2,400 waliokusudiwa; wakati uzalishaji wa mkonge utaongezeka kutoka tani 48,263 mwaka 2022/23 hadi tani 60,000 mwaka 2023/24.

Bashe alisema ongezeko hilo litatokana na mashamba mapya yatakayoanza kuvunwa katika msimu wa mwaka 2023/2024.

Alisema TSB itasambaza mbegu za mkonge bilioni 143 zitakazopandwa katika eneo la hekta 2,500 na itatoa mafunzo ya kilimo cha mkonge na ubora wa singa kwa wakulima wakubwa na wakulima wadogo.

Pia alisema TSB itatathmini mashamba ya wakulima wadogo ili kubaini majani ya mkonge yanayofaa kuvunwa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TSB, Saddy Kambona, alisema katika bajeti ya mwaka 2023/24, wanatarajia kupokea Sh. bilioni mbili zitakazowawezesha kununua mashine za kuchakata mkonge.

Kwa mujibu wa Kmabona, TSB itaanzisha mashamba ya vitalu, huku akisisitiza kuwa kutokana na kuwapo kwa mashine hizo fedha zitakazopatikana kutokana na uendeshaji zitaiwezesha TSB kununua mitambo mingi.

Pia TSB inatarajia kupokea Sh. bilioni mbili ambazo zimewawezesha kusambaza mbegu kwa wakulima bila malipo, kwamba kwa sasa wana hekta 60,000 za mkonge zilizo tayari kuvunwa.




Washiriki wa mradi wa Farm to Market Alliance (FtMA), wakiwa pamoja baada ya kumalizika mkutano wa kujadili teknolojia mpya ya iProcure inayowawezesha wakulima kutambua maeneo ya kuuza mazao yao, wilayani Babati mkoani Manyara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamiliki mgahawa wadai fidia mil. 365/-

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wawili wanaomiliki Kampuni ya Serengeti Holdings Ltd ya jijini Arusha, wametoa ilani ya siku 30 (notisi) kwa Halmashauri ya Jiji hilo kuilipa Sh. milioni 365 kwa kusababisha hasara kutokana na kuvunjwa kwa mgahawa wao kinyume cha utaratibu.

Aidha, wafanyabiashara hao wanakusudia kuipeleka mahakamani halmashauri hiyo iwapo itashindwa kulipa kiasi hicho cha fedha.

Wakili anayewawakilisha wafanyabiashara hao kutoka Kampuni ya Uwakili ya Caden Dante Attorneys, John Mallya, alisema jana kuwa ilani hiyo imeanza Mei 9, mwaka huu na itafikia ukomo Juni 9.

Kwa mujibu wa Mallya, wateja wake wamepata hasara hiyo kutokana na uharibifu, hivyo wanataka kulipwa fidia ya Sh. milioni 365. Alisema Septemba 7, 2007 halmashauri hiyo iliingia makubaliano ya upangaji na wateja wake na mwaka 2011, wateja wake waliwekeza mradi wa mgahawa wa gari linalotembea katikati ya Jiji la Arusha wenye thamani ya Sh. milioni 154.

"Huyu mteja wetu, tangu mwaka 2011 aliwekeza kwa kuweka gari/trailer maalumu la kusimama sehemu moja (trailer lenye majiko ya kisasa ya gesi, mitungi ya gesi, jokofu, na friza na vifaa vya kuzuia moto-fire sensor).

"Walijenga miundombinu ya kuwezesha kufanyika kwa biashara ya chakula ikiwa ni pamoja na jiko la kupikia pizza, banda la wateja, mabenchi, choo, matangi ya kuhifadhi maji, mtambo wa kuzalisha umeme wa jua, mtambo wa kufua umeme, miundombinu ya kutoa majitaka na wa akiba ya umeme.

Mallya alisema Mei 3, mwaka huu, halmashauri hiyo kupitia askari wake wa jeshi la akiba, walivamia eneo hilo na kufanya uharibifu, kwa madai ulijengwa kinyume na utaratibu wa mipango miji ya jiji hilo.

Kwa mujibu wa Mallya, katika utekelezaji wa operesheni hiyo, kulikuwa na mpango mchafu wa kibiashara wenye harufu ya rushwa.

"Mteja wangu alikuwa akiuza wastani wa Sh. milioni 1.6 kwa siku na alitoa ajira kwa Watanzania 15. Alikuwa akilipa mapato ya serikali bila usumbufu wowote. Kutokana na uharibifu huo, naitaka halmashauri hii kumlipa Sh. milioni 365 kama fidia ya mali zilizoharibiwa na hasara ya kibiashara," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Hargeney Chitukuro, alipotafutwa kuzungumzia jambo hilo, alisema uamuzi wa kubomoa mgahawa huo uliamuliwa na Kamati ya Mipango Mji ya Halmashauri hiyo.

"Si uamuzi wa mkurugenzi bali ni wa Kamati ya Mipango Miji. Wafanyabiashara hao waliombwa bila mafanikio kuwasilisha nyaraka mbalimbali za uhalali wa kuwapo kwao katika eneo hilo, lakini hawakufanya hivyo.

"Lakini eneo hilo si salama kwa biashara baada ya kuonekana kuna biashara ya kituo cha mafuta na benki. Alipewa kibali cha mgahawa wa kutembea, lakini yeye aliamua kufanya ujenzi wa kudumu katika eneo hilo na alipoombwa kibali hakutii amri hiyo, ndipo uamuzi wa kuvunja mgahawa ulipoamuliwa," alisema.

## Uamuzi wa pingamizi Ngorongoro Mei 15

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, itatoa uamuzi mdogo Mei 15, mwaka huu, kuhusu pingamizi la kisheria lililowekwa na Jamhuri katika kesi ya wanavijiji wa Loliondo wilayani Ngorongoro, Arusha wanaopinga zuio la kuingia kwenye Pori Tengefu la Pololeti lililowekwa na Waziri wa Maliasili na Utalii.

Kesi hiyo namba 21 ya mwaka 2022, ilifunguliwa mahakamani hapo kama maombi ya mapitio ya sheria (Judicial Review Application), dhidi ya tangazo la Waziri wa Maliasili na Utalii, kupitia (GN No 421).

Uamuzi huo mdogo utatolewa mahakamani hapo na Jaji Joachim Tiganga, anayesikiliza shauri hilo.


Kwa mujibu wa Wakili wa utetezi, Yonas Masiaya, wananchi hao wanapinga tangazo la waziri la kuwazuia kuingia katika ardhi ya vijiji vya Loliondo ambalo linadaiwa kuwa Pori Tengefu la Pololeti.

Katika shauri hilo, waleta maombi watano katika kesi hiyo kutoka vijiji vilivyoathirika, wanaiomba mahakama iagize serikali kuondoa zuio dhidi ya wananchi kuingia kwenye eneo la kilometa za mraba 21,502 ambalo wamekuwa wakitumia kwa ajili ya malisho ya mifugo yao na kufanyia shughuli za imani yao.

Pili, wanaiomba mahakama, itengue tangazo la serikali (GN 421) la Juni 17, 2022 kwamba ni batili na lilitangazwa kinyume cha sheria na halikuwashirikisha wananchi kama sheria inavyotaka.

Tatu, wananchi hao wanaiomba mahakama hiyo itamke kuzuia serikali na mawakala wake wasifanye operesheni zote kwenye eneo hilo.

Jamhuri katika kesi hiyo ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Jackline Kinyasi, inadai kuwa imeweka pingamizi hilo, kwa kuwa upande wa utetezi, haukuwasilisha jalada la kesi hiyo katika muda muafaka, hivyo walikuwa nje ya muda.





# Bil. 7.5/- kutatua kero za maji Kagera

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MIRADI 13 ya maji vijijini yenye thamani ya Sh. bilioni 7.5 inatarajiwa kuanza kutekelezwa hivi karibuni katika wilaya zote za mkoa wa Kagera baada ya mikataba kutiwa saini kwa lengo la kutatua kero za huduma hiyo katika maeneo mbalimbali ya vijiji katika mwaka wa fedha 2022/23.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Meneja Wakala wa Majsafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Kagera, Mhandisi Warioba Sanya, alisema tayari mikataba hiyo imetiwa saini na makandarasi wameanza kazi ambayo itasaidia kuongeza asilimia za upatikanaji wa maji kwa wananchi.

Mikataba hiyo, alisema imeongezeka kwenye shughuli za mwaka wa fedha 2021/22 ambazo zinaendelea kufanyika katika miradi mbalimbali ndani ya wilaya za Kagera ambazo kwa jumla ina thamani ya Sh. bilioni 11.2 kati Sh. bilioni 11.6 zilizopangwa kwa ajili ya kufanikisha mpango huo.

Pia alisema ndani ya miaka miwili imetiwa saini miradi ya Sh. bilioni 41.1 kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi wa mkoa huo na kufikisha asilimia 77 ya wananchi wanaofikiwa na huduma hiyo kwa sasa.

"Malengo ni kufikia asilimia 80 hadi 90, hivyo kufuatia miradi hiyo iliyotiwa saini tuna uhakika wa kufikisha huduma hii kwa asilimia tajwa na zaidi," alisema.

Amri Alhabisi, mkandarasi aliyetia saini mkataba wa kutekeleza miradi hiyo, alisema utekelezaji wake umeanza Mei, mwaka huu na unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, mwaka huu, kulingana na makubaliano yalivyopangwa na huduma hiyo kuanza kuwafikia wananchi katika maeneo yao.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alisema utiaji saini wa mikataba hiyo unategemewa kuwa na matokeo mazuri katika kazi kutokana na utendaji mzuri na kumtaka mkandarasi kutekeleza kwa wakati miradi hiyo ili kufanikisha lengo la serikali la kuwahudumia wananchi wake.

# Machinga wapigwa 'stop' siasa chonganishi

**Na Titus Mwombeki,** BUKOBA

WAFANYABIASHARA wadogo, maarufu kama Machinga mkoani Kagera, wamepigwa marufuku kujihusisha katika siasa chonganishi zisizo na tija ambazo zimekuwa zikiwaingiza katika migogoro ya mara kwa mara, hivyo kurudisha nyuma maendeleo yao.

Onyo hiyo lilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alipotembelea kiwanja kilichotolewa na Manispaa ya Bukoba kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za machinga katika Kata Kashai. Manispaa ya Bukoba, akiwa ameambatana na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Bukoba Mjini.

"Tumekuwa na machinga wengi ambao wanajitumbukiza katika siasa 'uchwara' ambazo haziangalii makuzi ya kiuchumi na kuwafanya kuwa daraja la wahujumu uchumi. Hatutaki hayo yaendelee maana Rais (Samia Suluhu Hassan) anawatambua na kuheshimu kazi yenu ndiyo maana ametoa fedha mjengewe ofisi na maeneo maalum ya kufanyia kazi," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa Rais Samia anachotaka kukiona ni ufanisi wa fedha alizozitoa kujenga ofisi hiyo iendane na thamani ya fedha zenyewe ili wawe na anwani na kutambulika kisheria.

Pia alitumia wasaa huo kukemea vitendo vya baadhi ya machinga ambao wamekuwa wakiendelea kupanga bidhaa zao katika maeneo ambayo si rafiki na kuhamia maeneo ambayo yamepangiwa na mkurugenzi wa manispaa hiyo ili kufanya biashara zao.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba, Hamid Njovu, akielezea upatikanaji wa kiwanja hicho, alisema kina ukubwa wa mita za mraba 434 baada ya kupokea maelekezo kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa.

Alisema mpaka sasa Rais Samia ameshatoa Sh. milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi za machinga, hivyo kazi hiyo itaanza muda si mrefu.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Machinga Mkoa wa Kagera, Evodius Rweyemamu, aliishukuru serikali kwa kutoa pesa zitakazosaidia ujenzi wa ofisi huku akisisitiza kuwa upatikanaji wa ofisi hiyo utasaidia machinga kuwa na utambulisho na kukopesheka hata kwenye taasisi za fedha.



Baadhi ya wakazi wa mtaa wa Bukondamoyo, kata Mhungula, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wakiwa wamepanga mstari juzi, kwa ajili ya kuchota maji yanayogharamiwa na Mbunge wa Kahama Jumanne Kishimba kila siku ya Jumanne katika kata za Mhungula, Nyahanga na Nyihogo ili kuwaondolea adha wananchi ya kutumia maji ya kwenye visima ambayo sio safi na salama.
**PICHA: SHABAN NJIA**

# Sungusungu wakanywa kujichukulia sheria mkononi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Janeth Magomi, ameliitaka Jeshi la Jadi la Sungusungu mkoani hapo kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi, bali wanapokamata wahalifu washirikiane na polisi kuwachukuliwe hatua zaidi za kisheria.

Alisema hayo juzi wakati akitoa mafunzo elekezi kwa Sungusungu Kata ya Ndala juu ya utendaji kazi, iliyoandaliwa na diwani wa kata hiyo, Zamda Shabani.

Kamanda Magomi alisema Jeshi la Polisi linatambua utendaji kazi wa Sungusungu katika kukabiliana na uhalifu, hivyo kuwasihi katika utekelezaji wa majukumu yao wasiwe wanajichukulia sheria mkononi na kuwaadhibu wahalifu, bali wafuate taratibu za kisheria.

"Sungusungu kiukweli mnafanya kazi nzuri katika kuhakikisha maeneo yetu, mali na watu wetu wote wanakuwa salama. Hii ni faida ambayo sisi Jeshi la Polisi tunaitambua na kuithamini sana. Niendelee kuwataka mfanye kazi hii huku mkitanguliza uzalendo na kufuata sheria za nchi," alisema.

Naye Diwani Shabani alisisitiza jeshi hilo la jadi kuendelea kushirikiana na viongozi katika kuhakikisha amani inatawala ndani ya jamii.

Katibu wa Sungusungu, Raymond Misana, alisema wataendelea kushirikiana na polisi kutokomeza uhalifu ndani ya jamii, huku akiahidi kufuata sheria za nchi na kuacha kujichukulia sheria mkononi.

Alisema katika kukabiliana na uhalifu wamezuia matukio makubwa ambayo yalikuwa yakijirudia mara kwa mara, yakiwamo wizi wa mifugo, kuvunja maduka na nyumba za watu na kuiba mali, uporaji wa simu za mkononi na mikoba kwa kutumia bodaboda.

Alitoa wito pia kwa wakazi wa Shinyanga kwamba katika nyumba zao wafunge taa za nje na wawe wanafunga milango au mageti kwa nyakati za usiku kwa sababu matukio mengine ya uhalifu yatokana na uzembe wa wananchi wenyewe.



Ukurasa 13

## RC ashika bango dai la ushoga mkoani, vikao madiwani kashfa zawasha moto




## Mwakilishi UNFPA: Kinga vifo vya wajawazito, 'vichanga' ni wakunga

Ukurasa 14

# Wadau Taasisi Moyo waanika ushindi kitaaluma, zao alilowekeza Rais Samia

## • Ujuzi kufika kila mkoa; ubia na Zambia, Rwanda...

**Na Christina Mwakangale**

ZAO la utekelezaji wa ahadi kazi ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuelekeza uwekezaji katika taaluma kutoka nguzo ya hospitali kubwa, sasa sekta ya afya yaanza kuchukua sura pana ya ufaulu, pale mfumo wa ushirikiano kimataifa, ukibeba majibu ya kina katika wajibu wa hospitali hiyo maalum.

Ni hivi karibuni, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), imetia saini mkataba wa miaka mitatu ya makubaliano na Hospitali ya King Faisal ya nchini Rwanda na Hospitali ya Taifa ya Moyo, nchini Zambia, kutibu wagonjwa wa moyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dk. Peter Kisenge (kulia) na Naibu Mtendaji Mkuu Hospitali ya King Faisal ya nchini Rwanda,Frederic Ngirabacu, wakionyesha mkataba wa kutibu wagonjwa wa moyo na kuwajengea uwezo wataalamu wa tiba hiyo.**PICHA: JKCI.**

Mbali na matibabu pia mkataba huo unahusisha ujenzi wa uwezo wataalamu wa afya wa hospitali kutoka nchi hizo, ikiwa ni mpango unaowezeshwa na Shirika la Okoa Moyo wa Mtoto Save a Child's Heart (SACH) la nchini Israel, ambalo limejikita kwenye utoaji huduma na upatikanaji wa matibabu ya moyo nchini na kwa ujuzi kwa nchi mbalimbali za Afrika.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dk. Grace Magembe, mgeni rasmii kwenye hafla hiyo ya utiaji saini, anasema ni azma ya serikali ya Rais Dk. Samia, kuhakikisha kwamba huduma za afya nchini inakuwa sehemu ya utalii, huku nchi za Afrika zikivutiwa na huduma hizo na kuja kutibiwa.

Anasema, serikali iliyoko madarakani chini ya Rais Dk. Samia, imepiga hatua katika sura ya kuwekeza vifaa tiba na miundombinu, pia dawa za kuwezesha ufanisi wa hudunma hizo za kiafya ziimarike nchini.

"Huduma ya afya kiutalii ndio mkakati wa nchi na Rais Samia, baada ya kuwekeza kwenye rasilimali watu. Taasisi hii imekuwa ni kati ya zinazoaminiwa barani Afrika na huduma za JKCI zitaifikia mikoa yote kutoa uzoefu kwa madaktari wa hospitali zingine," anasema Dk. Maghembe.

Anafafanua kisekta kuwa, nia ya rais sasa ni kupunguza idadi ya rufani ambazo hupatiwa wagonjwa kwa ajili ya tiba nje ya nchi, ambazo zina gharama kubwa, sasa zipatikaneJKCI.

**WENYE JUKUMU**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa JKCI, Prof. William Mahalu, anasema hatua iliyofika taasisi hiyo ni kubwa, akisema anachokishuhudia katika utendaji wa matibabu bobezi na kibingwa ni ndoto yake kutimia.

"Wakati nafikiria kuanzisha taasisi ya moyo, kila mmoja aliniona napoteza muda. Nashukuru Mungu kunipa uhai na kushuhudia hiki leo, kwa sababu wapo walionikatisha tamaa kwamba taasisi ya moyo sio kipaumbele. Tujitahidi kufanya vitu wenyewe haijalishi kwa udogo gani. Upasuaji tufanye wenyewe," anasema Prof. Mahalu.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, anasema SACH ya Israel imekuwa ikiwasaidia watoto wenye magonjwa ya moyo kupata matibabu pamoja na kuwapa ujuzi madaktari wa JKCI, kwa ushirikiano tangu mwaka 2015.

Anasema shirika hilo lilianza kwa kuwachukua watoto wenye magonjwa ya moyo ambayo hayakuweza kutibiwa hapa nchini na kuwapeleka nchi ya Israel, kwa ajili ya matibabu na sasa JKCI imekuwa na uwezo wa kutibu magonjwa hayo, ndio maana nchi za Rwanda na Zambia zimefika nchini, ili nazo ziweze kupata ujuzi huo.

"Shirika la Okoa Moyo wa Mtoto la nchini Israel, limekuwa likiwahudumia watoto wenye magonjwa ya moyo wanaotoka katika familia duni kuokoa maisha yao na pale walipohitaji kuwapeleka nchini Israel walifanya hivyo kwa upendo," anasema Dk. Kisenge.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Okoa Moyo wa Mtoto (Save a Child's Heart - SACH) la nchini Israel Simon Fisher, anasema hatua iliyofikia hadi Rwanda na Zambia kukubali kutia saini mikataba hiyo, imetokana na ushirikiano wa muda mrefu uliopo kati ya SACH na JKCI.

"Leo hii Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete inafanya upasuaji mkubwa wa moyo, pamoja na upasuaji wa tundu dogo kwa watoto kwa kujitegemea naamini baada ya miaka kadhaa wenzetu wa Rwanda na Zambia nao watakuwa na uwezo huo", anasema Fisher

**WADAU WASHIRIKA**

Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Moyo ya nchini Zambia, Dk. Shumba Chabwela, anasema kutia saini mkataba wa makubaliano ya kutibu wagonjwa wa moyo pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa afya wa nchini Zambia, kunaonyesha utimilifu wa ushirikiano uliojengwa na waasisi wa nchi za Tanzania Mwalimu Julius Nyerere na wa Zambia Kenneth Kaunda.

"Kwa niaba ya nchi ya Zambia tunatoa shukrani zetu za dhati kwa kutupa nafasi ya kushirikiana nasi kuwahudumia wagonjwa wetu, kabla hata ya kusaini mkataba huu tayari tulishaanza kuleta wataalamu wetu kujifunza katika Taasisi hii", anasema Dk. Shumba.

Naibu Mtendaji Mkuu Hospitali ya King Faisal ya nchini Rwanda, Frederic Ngirabacu, anasema ushirikiano katika sekta ya afya na sekta nyingine vinapaswa kufanyika baina ya nchi za Afrika ili kwa pamoja ziweze kukuwa na kuacha kutafuta huduma katika mataifa ya mbali.

"Tumeanza ushirikiano na JKCI wiki hii lakini pia tumefurahi kukuta waafrika wenzetu kutoka Zambia wanashirikiana nao, hii inaonyesha ukomavu katika nchi zetu za Afrika", anasema Ngirabacu.

Kwa mujibu wa Naibu Mkurugenzio huyo, Shirika la Okoa Moyo wa Mtoto la nchini Israel, limekuwa likisaidia kutoa huduma za matibabu ya moyo kwa watoto wenye magonjwa ya moyo waliopo nchini Rwanda na sasa linawaunganisha na JKCI, ili kuendeleza ushirikiano, jambo ambalo hawakulitarajia hapo awali.

MAZINGIRA

STADI ZA KUSAFISHA NYUMBA...

# Wanafunzi sekondari wabuni chombo kinachofyonza vumbi kielektroniki

• Wasifu; gharama nafuu, kusiko umeme kinatumika




Wanafunzi wa Shule ya Sekondari St Peter Claver, iliyopo Ihumwa, Dodoma wakiwa katika maonyesho ya Wiki ya Ubunifu, iliyomalizika hivi karibuni, katika Uwanja wa Jamhuri, mjini Dodoma. **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU.**

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI inasisitiza kuibuliwa vipaji mbalimbali kwa vijana chipukizi wa kike na kiume, ili kuviendeleza vilete matokeo chanya kitaifa, ikiwamo kuwaandaa wajiajiri, huku mwelekeo kisera nao ukichukua njia hiyo.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolijia, kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) katika kutekeleza hilo imekuwa ikiandaa mashindano yaitwao MAKISATU yanayoenda sambamba na Wiki ya Ubunifu kitaifa.

Lengo ni kuibua vipaji vya wabunifu wachanga, pia zitambulike kitaifa na kimataifa kuja kuonyesha bidhaa zao, zinazoshindanishwa katika kundi husika, kumsakla mshindi, pia ikiwa ni namna ya kuvutia wabunifu wachanga kujitokeza kuwasilisha mawazo yao yafanyiwe kazi, sasa kukionekana mafanikio.

Katika mashindano hayo, nafasi ya kwanza mwaka huu imeenda kwa Chuo cha Ufundi Arusha au Arusha Tech, ya pili Shule ya St, Peter Claver, ambayo ubunifu wake ulijikita kwenye kifaa cha kusafisha mazingira, kufyonza vumbi kwa njia ya kielektroniki.

**UBINIFU ULIVYO**

Mmoja wa timu ya wabunifu, Patricia Mhilu anayesoma kidato cha nne, anasema waliamua kubuni mfumo huo kurahisisha jamii kuweka mazingira safi, katika maeneo wanayoishi na ofisini.

Kwa mujibu wa Patricia akizungumza, sababu kubwa iliyowafanya wabuni mashine hiyo ya kuondoa vumbi, ni kutaka jamii kuweka mazingira safi kwenye nyumba wanazoishi na maeneo mengine, kutokana na kuwapo changamoto ya vumbi inayoleta athari nyingi za kiafya.

Anasema wakaanza kwa utafiti mdogo kudadisi tatizo lililoko, wakarejea shuleni na kubuni njia mbadala inayosaidia kuondoa vumbi, badala ya kutumia vitambaa kufuta kama ilivyozoeleka kwa jamii nyingi. Hapo ndio ukawa mwanzo wa kufyonzwa na kusafishwa vumbi.

"Sehemu kubwa ya jamii inatumia vifaa kama vitambaa kwa ajili ya kukung'uta vumbi, suala ambalo linatumia muda mrefu. Lakini, ukitumia mashine hiyo, inakusaidia kutumia muda mchache kusafisha sehemu kubwa ya mavumbi yaliyopo ndani," anasema Patricia.

> **Hapo anafafanua kwamba, wamebuni wazo na wamelifanyia kazi kwa kuonyesha mashine, sasa wanaiomba serikali kufuatilia ubunifu waliol nao uendelezwe na Kutambulika, kwa manufaa ya sasa na baadae.**

Hapo anafafanua kwamba, wamebuni wazo na wamelifanyia kazi kwa kuonyesha mashine, sasa wanaiomba serikali kufuatilia ubunifu waliol nao uendelezwe na Kutambulika, kwa manufaa ya sasa na baadae.

Mwanafunzi Victoria Nchilla, anasema mashine walioibuni ya kufyonza vumbi, hadi sasa ina faida kubwa kwa kwa jamii, akiisifu ina gharama nafuu, nzuri na inaweza kutumika sehemu yoyote ile, kutokana na kutumia betri na umeme ili kuweza kufanya kazi.

Anasema ni mashine inayoweza kutumika kwa wakazi wa vijijini na mjini, kwa sababu inatumia betri, hata kuwafaa jamii iliyoko vijijini, ambayo bado haijaunganisha umeme kwenye makasio yao.

"Hii bunifu ni nzuri sana na inahitaji kuendelezwa ili iweze kupiga hatua na kutambulika kimataifa, kwa sababu ina faida kubwa na inaweza kutumika mijini na vijijini," anasema Nchilla.

**MAMLAKA YA SHULE**

Buberwa Karongo ni Mkuu wa Shule anasema shule inatambua umuhimu wa vipaji vya wanafunzi na ndio maana wamewaruhusu kwenda kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya ubunifu, ili wajifunze zaidi kutoka kwa wanafunzi wa shule nyinginezo.

Karongo anafafanua, pia wanahitaji kuona mwanafunzi anakuwa mzuri katika masomo ya vitendo nje ya darasani na ni moja ya sababu zao, kuwapa elimu ya ubunifu vijana hao, wakiwaandaa kujiajiri katika mustakabali wa baadae.

Pia, mkuu huyo wa shule, anaishIkuru serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolijia, kwa kuandaa Wiki ya Ubunifu, akiamini inasaidia kuwajenga vijana katika somo la ubunifu, ambalo hulifanya kwa vitendo, kutokana na mawazo yao wanayayowasilisha kwa walimu yakaidhinishwa, kabla ya kuwasilishwa katika Maonyesho ya Wiki ya Ubunifu.

Anasema ni hali inayosaidia kuwajengea uwezo wanafunzi, ikiwamo kuwapa muda wa kubadilishana mawazo na wanafunzi wa shule nyinginezo, kitendo kinachowasaidia kupanua wigo wa ubunifu ambao unapoendelezwa, unarejesha matokeo chanya kwa wote.

Mkuu wa Taaluma wa shule hiyo, Jeannette D'mello, anaishauri serikali kutenga bajeti kwa wanafunzi wa shule za sekondari wenye uwezo kubuni mifumo ya kuondoa changamoto kwa jamii, ili kuwasaidia kukuza vipaji vyao na kuingia kwenye soko la ushindani.

D'mello anasema, vipaji vya wanafunzi wanavyovionyesha katika makongamano na wiki za ubunifu katika maeneo mbalimbali wakiwa bado chipukizi, kama walivyofanya vijana wake, inapaswa kuendelezwa kadri siku wanavyozidi kukua.

Anasema shule yake ina dira ya kumtengeneza mwanafunzi katika nyanja tofauti, ikiwamo iliyobnazishwa ya usafi wa mazingira, kwa ajili ya faida yake siku zijazo. Anendelea: "Tumekuwa tukiwafundisha darasani wanafunzi wetu kwenye kitengo cha Sayansi na vitengo vingine, wanafunzi wamekuwa wakibuni vitu mbalimbali na walimu kuwasimamia, ili ubunifu wao uboreshwe na kuingia katika mashindano au maonyesho ya ubunifu,"

**WAZIRI PROF. MKENDA**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, anawataka wabunifu kutobweteka na ushindi walioupata, badala yake wapige hatua zaidi, kwa kile walichokibuni mwaka huu, ili mwakani kiweze kuendelezwa na kufikia ngazi ya kimataifa.

Profesa Mkenda anayasifu maonyesho ya sasa, yamekuwa bora zaidi, kwa sababu wengi walioshirikishwa, ubunifu wao ama umetimia au ulishaendelezwa na serikali na kutambulika kimataifa, hivyo wasisite kubuni bidhaa bora wawavutie wabunifu wachanga kujitokeza katika maonyesho tajwa.

AFYA

# RC ashika bango dai la ushoga mkoani, vikao madiwani kashfa zawasha moto

**Na Neema Hussein, MPANDA**

SASA ni kilio kinachukua nafasi kitaifa, pale kilio cha ukatili, mahsusi mapenzi ya jinsia moja, sasa ikitua kwenye Baraza la Madiwani la Manispaa ya Mpanda, dai likiwa ni ukatili huo kwa wingi majumbani.

Ofisa Maendeleo katika Manispaa ya Mpanda Marietha Mlozi, anasema sasa hivi kuna tafsiri kubwa ya ukatili kutokana na kupanuka maana halisi ya vitendo hivyo, kinyume na zamani, unyanyasaji wa namna hiyo uliwaendea zaidi watoto na wanawake.

Marietha analalamika kwamba, wimbi kubwa la ulawiti wa watoto wa kiume liko juu, huku kuna watoto wanaolawitiana wenyewe na wengine wanalawitiwa na watu wazima. Hapo anafafanua: “Ukatili kwa kiwango kikubwa, karibu asilimia 60 inaonekana unatokea kwenye makazi yetu, yaani majumbani, wale watu tunaowaamini tunaoishi nao, tunafikiri ni watu wema, lakini ndio wanaofanya ukatili kwa watoto wetu.

“Sasa wito wangu ni kwamba tujitahidi kutowalaza watoto na wageni, haijalishi ni mchungaji, kaka yako, haijalishi ni binamu yako, usimlaze mtoto kando na wageni sababu hujui undani wake!”

Akijibu swali katika kikao cha Madiwani Manispaa ya Mpanda, Ofisa Ustawi Jamii ananena:”Mheshimiwa Mwenyekiti (Meya Baraza la Madiwani), hili tatizo la ulawiti kwa watoto nimeulizwa swali kwamba kuna viashiria gani katika kugundua ukatili huo nimeeleza kwamba sio viashiria haya mambo yapo kabisa hapa Mpanda na yanatendeka.

“Na yanatendeka kwa watoto wetu wa shule za msingi na sekondari na ninaomba nitoe mfano, kama wiki mbili zilizopita tumepata tukio la mtoto wa kiume kutoka shule moja ambayo sitaitaja, ambaye amekuwa anafanya biashara ya ngono ya jinsia moja.

“Kwa maana kwamba huyo mtoto yuko kidato cha pili, anakuwa na marafiki wanaume na niwatu wazima na familia zao na walikuwa wamekamatwa kama watano wamewekwa ndani, sijafuatilia kwa karibu hapa kwamba wamefikia wapi, kama wamepewa dhamana na kesi imefikia wapi.

“Kwa hiyo, hili tatizo lipo kubwa kama nilivyosema awali. Pia, tuna mtoto mmoja wa shule ya msingi hapa Mpanda darasa la nne ana miaka 11, amekuwa akiwafanyia hivyo vitendo watoto wenziwe...sasa wito wangu... kwetu sisi wote kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2019 Kifungu cha 95, Kifungu Kidogo cha Kwanza, kinasema kila mtu ana wajibu wa kumlindamtoto.



Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko

“Nieleze, vyanzo vya ukatili ni nini? Tafiti zilizofanyika, zinaonyesha vyanzo vya ukatili ni pamoja na malezi hafifu ya wazazi na walezi wa watoto. Hatutoi elimu kwa watoto, hatuzungumzi na watoto, watoto wanaishi maisha yao wazee wa zamani, walikuwa na hekima sana na akili. Walikuwa wanawasha moto jioni wanakaa wanazungumza na watoto wao, sisi tumekua kidigitali zaidi, tuko ‘bize’ kuchati na simu na kutafuta fedha.

“Tunatarajia kuwa na kizazi gani? Watoto ndio hatima yetu, ndio tunatarajia kuwarithisha nchi hii ya Tanzania. Tutafanya miradi mingi, tutafanya mambo mengi, lakini tusipokuwa na kizazi chenye tija, sawasawa na bure,” anatamka Marietha.

**MEYA NA YAKE**

Meya wa Manispaa ya Mpanda, Haidary Sumry, anatanguliza kazi kupitia kikao hicho amempongeza Mkuu wa mkoa wa Katavi Mwanamvua Mrindoko kwa jitihada kubwa na nzuri ambazo anazifanya hasa katika eneo la mapenzi ya jinsia moja.

“Mkuu wa Mkoa yuko mbele zaidi yetu, amechukua hatua nyingi, lakini nipongeze pia kamati za ulinzi na usalama za mkoa na wilaya, wamechukua pia hatua nyingi na kubwa ambazo zinafanyika. Mpaka sasa hivi tunajua hali iko vipi na kuna wenzetu ambao hawajalala kwa ajili ya kufuatilia haya mambo.

“Ukweli usiopingika alivyoongea ofisa wetu (ustawi jamii) kwamba jambo hili kwenye Manispaa yetu lipo, sio kwamba halipo. Tushirikiane na viongozi wetu hapa mkuu wa mkoa, wakuu wa wilaya, viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama na tunashirikiana nao kwa njia gani hata kwa kuwapa taarifa.

“Sababu, kazi zetu viongozi wakati mwingine jambo linaweza kuwa linausiri unapenyeza zile taarifa unazozipata sababu sisi tunakaa huko tunajadili,tunakaa kwenye makundi mbalimbali wanasiasa tunakaa kwenye vijiwe vya kahawa tunasikiliza.

“Kama kuna ‘NGO’ (taasisi zisizo za kiserikali) zozote ambazo zipo kwenye manispaa yetu (Mpanda) ambazo zinajihusisha na haya mambo ambayo tunayaongelea hapa, mapenzi ya jinsia moja sio rahisi mkuu wa mkoa kujua.

“ Sio rahisi mkuu wa wilaya kujua, ila kupitia sisi taarifa ambazo tutakuwa tukizipenyeza kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, zinaweza zikasaidia kujua na hatua zikachukuliwa, hatimaye tukalipunguza hili tatizo na baadae tutaenda kulitokomeza kabisa,” anasema Meya huyo, akiongoza kikao cha madiwani.

**NYENDO NA UZOEFU WA RC**

Mkuu wa mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, amekuwa akitumia muda wake kuzungumza na wananchi pale anapokutana nao, kuhusu vitendo hivyo vya ukatili unaojitokeza, lengo ni kuhakikisha wananchi wanachukua hatua, hatimaye kupunguza au kutokomeza kabisa suala la ukatili na mapenzi ya jinsia moja katika mkoa wa Katavi na Tanzania kwa ujumla.

Ni hivi karibuni, Nipashe lilimshuhudia mkuu huyo akizungumza na wakazi wa Nsimbo, kuhusu adha hiyo ya kijamii, akiwatamkia: “Niwakumbushe suala la mmomonyoko wa maadili, maana kila ninapokutana na wananchi, lazima hili nilizungumze. Ndugu zangu wananchi wa mkoa Katavi mliopo hapa Nsimbo, tuna tatizo sasa hivi la mmomonyoko wa maadili kwenye jamii zetu.

“Na sio kwamba haya mambo tukiyasikia redioni, kwenye televisheni, magazetini au kwenye mitandao, tukafikiri sisi mkoa wa Katavi hatuhusiki, tunahusika kwa asilimia kubwa.Vitendo vya ubakaji vipo na vinaongezeka, vitendo vya jinsia moja kwa maana ya ushoga na usagaji vipo, tumefanya uchunguzi na ufuatiliaji wa awali tumebaini vipo.

“Watoto wetu wanafanyiwa pia wanafanyiana wenyewe kwa wenyewe, lakini hata watu wazima wapo waliojitoa akili na wamejiingiza kwenye vitendo hivyo. Mimi niseme tu, hayo sio maadili ya Kitanzania. Kwa watanzania wanaofahamu namna ambavyo nchi yetu ni nzuri na inaheshimika, ina amani, utulivu na maadili yake.

“Tuhakikishe tunalikataa vikali jambo hili la ndoa za jinsia moja, vitendo vya ubakaji na mambo mengine ya ukiukwaji wa maadili ya Kitanzania. Ukiona kuna dalili za jambo kama hilo, usisubiri likatokea ndio ukaanza kuchukua hatua, toa taarifa na chukua hatua zinazostahili kuhakikisha jambo hili haliendelei.

“Tusipokataa ushoga na usagaji ndugu zangu, tunakwenda kuangamiza kizazi chetu na baadaye kutakua hakuna watoto, watu watakuwa wanakwenda mwanamke kwa mwanamke, mwanaume kwa mwanaume, hakuna kizazi taifa linaangamia.

“Tusikubali siasa za namna hiyo, tusikubali misaada inayoambatana na mambo hayo. Tuendelee kulinda mila zetu, maadili yetu na desturi zetu nzuri, ambazo pia kwenye dini zetu tumeendelea kufundishwa,” anasema Mkuu wa Mkoa Mwanamvua.

Mkurugenzi wa taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya Usevya Development Society (UDESO), Eden Waymba, wakati akifungua mafunzo ya kamati zake, akagusia, suala hilo anatoa maoni yake kwamba: “Kama taasisi tunaomba nyie mlioko hapa kama kamati za PETS ambazo mmechaguliwa kutoka kwenye vijiji vyenu, mshirikiane na serikali kupambana na ukatili, pamoja na masuala ya ushoga.”

Anashauri kamati hiyo ishirikiane kuelimisha jamii, ili iwe salama katika kupambana na unyanyasaji kijinsia na ushoga.



Madiwani wilayani Mpanda, wakiwa kikaoni. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

AFYA

# Mwakilishi UNFPA: Kinga vifo vya wajawazito, 'vichanga' ni wakunga

**Na Yasmine Protace**

WAKUNGA kitaaluma wanaangukia kundi la wauguzi wanaopatiwa mafunzo maalum, kuwahudumia wajawazito wakati wa kujifungua na katika kuthamini utaalamu wao, wana siku maalum wanayoshereheka kimataifa, kila Mei, 5 ya mwaka.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Mark Bryan Schreiner, anasema dunia inashuhudia mwanamke akifa kila baada ya dakika mbili kutokana na ama ujauzito au kujifungua.

Schreiner anasema, UNFPA wanachukua hatua kupigania wakunga wajuzi, ikiwa ni njia muhimu ya kuepusha vifo vinavyozuilika vya uzazi na watoto wachanga. Hapo anafafanua:"Ikiwa kila mwanamke mjamzito angeweza kupata mkunga aliyefunzwa vizuri, anayejali, tungekuwa karibu zaidi na ulimwengu ambapo kila uzazi ni salama."

Anasema, kuna uhaba wa wakunga 900,000 duniani, huku kukiwapo dhana kwamba hao si wafanyakazi muhimu wa afya, lakini yeye anawasifu kuwa ndio wanaotoa taarifa muhimu za kiafya afya ya ngono na uzazi, kupanga uzazi na kuwasaidia wanakabiliana na masuala nyeti ya uzazi.

Pia, anawataja wakunga mara nyingi ndio wahudumu wa afya muhimu katika maeneo magumu kufikiwa, huku akiangalia upande wa pili wa shilingi,

kwamba madhara ya kuwakosa yanatisha ikiwamo vifo vya uzazi imesimama.

"Kila mwaka, wanawake 287,000 duniani kote hupoteza maisha wakati wa kujifungua; watoto wachanga milioni 2.4 hufa na wengine milioni 2.2 huzaliwa wakiwa wamekufa." anasema.

Anasema nchini Tanzania, wanawake 8,000 hadi 11,000 hupoteza maisha wakati wa kujifungua kila mwaka (takriban 30 kwa siku) na zaidi ya watoto 40,000 wanaozaliwa hawataona siku yao ya kuzaliwa.

"Haifai kuwa hivi! Upatikanaji wakunga kwa wote unatoa suluhisho bora na la gharama nafuu kukomesha vifo vya uzazi vinavyoweza kuzuilika. Kwa kufunga nakisi ya idadi ya wakunga, tunaweza kuzuia theluthi mbili ya vifo vya uzazi na watoto wachanga, kuokoa maisha ya zaidi ya milioni 4.3 kwa mwaka ifikapo 2035," anasema, akitaja kaulimbiu ya mwaka huu "Pamoja tena: kutoka kwa ushahidi hadi uhalisia."



Mwakilishi wa UNFPA nchini Tanzania, Mark Bryan Schreiner, akizungumzia jambo katika maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani.

Anafafanua kwamba nchini Tanzania, UNFPA imeendelea kushirikiana serikali kupitia Wizara ya Afya Bara na Zanzibar kuimarisha elimu ya ukunga, udhibiti, ushirika na mazingira wezeshi kwa vitendo vya ukunga, ikijumuisha uboreshaji vifaa vyao kwa vituo 64, mapitio ya mitaala ya uuguzi na ukunga na nyenzo za usaidizi.

Anaongeza kuwa UNFPA kwa kushirikiana na wadau wa TAMA, Wizara ya Afya, na Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto, Mtoto na Vijana (RMNCAH) wanaadhimisha tukio hilo kwa kufanya mjadala huo wa Jedwali la Duara kuhamasisha uwekezaji na kusaidia kupunguza vifo vya mama na watoto wachanga nchini Tanzania.

"Kupitia kuimarisha elimu na mafunzo ya ukunga kwa kuzingatia waelimishaji wakunga ni matumaini yangu kwamba jedwali hili la mzunguko litaongeza dhamira ya serikali na washirika kuwekeza katika uzalishaji, usambazaji na uhifadhi wa waelimishaji wakunga waliohitimu na wenye uwezo," anasema.

**RAIS WA WAKUNGA**

Rais wa Chama Cha Wakunga Tanzania, Freddy Mwanga, anasema maana ya Siku ya Kimataifa ya Wakunga, wanakusanyika kusherehekea taaluma na kutambua jukumu lao katika kuhakikisha uzazi salama na wenye afya kwa wanawake na watoto wachanga wanaozaliwa kote duniani.

Anasema ni tukio la kuthibitisha uhusiano na wadau na washirika, akiitaja kaulimbiu ya mwaka huu 'Pamoja Tena kutoka Ushahidi hadi Uhalisi,' inayozungumzia umuhimu wa kufanya kazi kwa ushirikiano, ili kuziba pengo kati ya ujuzi wao; bora wa ukunga na uhalisia wa kinachopatikana kwa sasa katika sehemu nyingi za dunia.

Mwanga anasema Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine zinazoendelea, elimu na huduma ya wakunga inakabiliwa na changamoto ya ubora wa huduma hizo, akitaja suala la kukubalika kwao tata na hivi karibuni kumekuwapo maendeleo wakunga wengi wakipewa mafunzo na kupelekwa vijijini, maeneo yenye uhitaji.

"Kwa ujumla, nchini Tanzania wakunga wanaohitimu kutoka shule za uuguzi na ukunga wanahitaji mafunzo ya ziada ya huduma na ushauri, ili kupata umahiri unaohitajika na kufanya mazoezi ya ukunga kwa usalama. Kwa hiyo, katika hatua hii tujikumbushe kwamba si kila anayejifungua ni mkunga (kama ilivyozoekeka)..."

Anasema, mkunga sahihi anapaswa kuwa na ujuzi ulioainishwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, Shirikisho la Kimataifa la Wakunga na kukidhi Fasili ya Mkunga na ICM iliyoidhinishwa na Shirika la Afya Duniani.

"Mkunga ni mtu ambaye amemaliza kwa mafanikio programu ya elimu ya ukunga ambayo imezingatia umahiri muhimu wa ICM kwa mazoezi ya ukunga na mfumo wa 'ICM Global Standards for Midwifery Education' na inatambulika nchini ilipo, ambaye amepata sifa zinazohitajika ili kusajiliwa," anasema.

Anafafanua kwamba inamaanisha si tu kuwapa maarifa na ujuzi muhimu, bali na kuwatayarisha kuwa watoa huduma wenye huruma, na wanaojali utamaduni. Anaendelea: "Ili kufikia lengo hili, ni lazima tuwekeze katika maandalizi ya walimu wakunga bora ambao nao watazalisha wakunga wenye uwezo.

"Tunahitaji kuhakikisha kwamba walimu hawa wanapata fursa zinazoendelea za maendeleo ya kitaaluma na waweze kuendana na maendeleo ya hivi punde katika utunzaji wa wakunga."

Anaongeza kwamba, wanahitaji kutambua kwamba utunzaji wa wakunga hauwezi kuwapo kwa kutengwa na kunahitajika kufanywa kazi kwa karibu na watoa huduma wengine wa afya, watunga sera na viongozi wa jamii ili kuandaa mazingira wezeshi kwa huduma ya wakunga.

"Hii ni pamoja na kushughulikia masuala ya kijamii, kiutamaduni na kiuchumi ambayo yanaweza kuzuia upatikanaji wa huduma kwa wanawake, pamoja na kutetea sera na programu zinazounga mkono elimu na mazoezi ya ukunga," anaeleza Rais huyo wa wakunga.

Mwanga anafafanua hoja yake kwamba, lengo ni kuwaandaa wakunga wenye uwezo watamkaofanya utambuzi wa ama kupunguza au kutokomeza vifo vinavyoweza kuzuilika vya uzazi na watoto wachanga.

Anatumia mfano wa takwimu za Utafiti wa Afya ya Demografia Tanzania (TDHS), unaotaja mwaka 2022 vifo vya watoto wachanga vilikuwa 24 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai.

Kurejea Mwenendo wa Makadirio ya Uwiano wa Vifo vya Uzazi (MMR), na UNDESA/Divisheni ya Idadi ya Watu Kanda, mwaka 2000 hadi 2020, vifo vya uzazi vilikuwa 429 kwa mwaka 2015 na mwaka 2020 vilikuwa 351, vifo vingi ni vinavyozuilika, kama vile kuvuja damu, shinikizo la damu na maradhi maambukizi.

"Hali hii inaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 10 zinazoongoza kwa mzigo mkubwa wa vifo vya uzazi na watoto wachanga. Ingawa kiwango cha utoaji wa huduma katika vituo vya kutoa huduma kimeongezeka kutoka asilimia 60 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 80 mwaka 2021 (Ripoti ya DHIS2), wanawake wanaojifungua katika vituo vya afya mara nyingi hawapati huduma bora zinazohitajika kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO)," anasema.



Wakunga wakifuatilia hafla ya siku yao. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE.**





# Timu kuchunguza migogoro ya ardhi

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, ameagiza kuundwa timu ya kuchunguza chanzo cha kukithiri kwa migogoro ya ardhi wilayani Kondoa mkoani hapa.

Agizo hilo limetokana na kuwapo malalamiko mengi ya wananchi kudhulumiwa maeneo yao na baadhi ya watumishi wa Idara ya Ardhi.

Dk. Ndumbaro aliagiza hayo juzi wilayani hapa alipozuru kwa lengo la ukagua maendeleo ya Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria inayojulikana kama Mama Samia Legal Aid.

Alisema kuwa kutokana kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wakidai kudhulumiwa maeneo yao, atatuma timu hiyo ambayo itakwenda kufanya uchunguzi kuhusu madai hayo.

"Ninaagiza tume kuja hapa kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko yenu kwa sababu kwa kiasi kikubwa wengi mmelalamika kuhusu migogoro ya ardhi. Wachache wamelalamika kuhusu masuala mengine yanayohusu haki jinai.

"Tume hii itakapokuja itashirikiana na uongozi wa wilaya kufuatilia na kusikiliza wananchi wote zaidi. Hata tulivyofanya leo (juzi) ili kuja na majibu na niwahakikishie kuwa mtumishi yeyote ambaye atabainika kuhusika na tuhuma za kudhulumu wananchi ardhi, tutamchukulia hatua kali ikiwamo kumfukuza kazi na kumfunga jela," alionya.

Dk. Ndumbaro alisema serikali haitokuwa tayari kuwavumilia watumishi ambao wamepewa dhamana ya kuwatumikia wananchi na wao kugeuka kuwa kikwazo kwa jamii.

"Muda wa watumishi wa aina hii haupo tena katika serikali hii. Ni wakati sasa wakaondoka na ninawaahidi siku hiyo mara baada ya tume hii kufanya kazi yake nitakuja pamoja na Waziri wa Ardhi na Kamishana wa Ardhi. Mtumishi yeyote atakayebainika, tutaondoka naye kwenda kumshughulikia,"alisisitiza.

Akizungumzia Kampeni ya Msaada wa Kisheria, waziri huyo alisema lengo lake ni kutoa elimu na msaada wa kisheria kwa wananchi ambao wamekuwa hawafahamu ni jinsi gani wanaweza kupata haki zao.

"Kampeni hii ilizinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na itadumu kwa muda wa miaka mitatu ikihusisha utoaji wa elimu ya sheria na msaada wa kisheria kwa wananchi wote Tanzania," alisema.

Alibainisha kuwa Mkoa wa Dodoma umekuwa wa kwanza kutekeleza kampeni hiyo na baadaye mikoa ya Shinyanga, Manyara na Ruvuma itafuata, lengo likiwa ni kuwafikia wananchi wote hadi Tanzania Zanzibar.

Mmoja wa wakazi wa Kondoa, Maulid Shana, aliishukuru serikali kwa kuanzisha kampeni hiyo ambayo itakuwa msaada kwa wananchi wengi ambao wamekuwa wakipoteza haki zao kwa kukosa msaada wa kisheria.

# Wabunge waibana serikali wanafunzi kusoma kwa zamu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wamehoji mikakati ya serikali kuondoa tatizo la wanafunzi kusoma kwa zamu katika baadhi ya shule, ikiwamo katika Halmashauri ya Mji wa Tarime.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge wa Tarime Mjini (CCM), Mwita Kembaki, alisema kuna shule inayoitwa Buhosi ina wanafunzi zaidi ya 1,000 na kuna madarasa sita na kuhoji lini serikali itatenga fedha za kutosha kujenga madarasa ya shule hiyo.

"Zipo jitihada za wananchi wanazofanya za kujenga shule mpya, lakini serikali haijapeleka fedha kukamilisha ujenzi huo. Lini fedha zitapelekwa kukamilisha majengo hayo?" alihoji.

Mbunge wa Viti maalum (CCM), Fatuma Toufiq, alisema Shule ya Msingi Kizota ni miongoni mwa shule zenye wanafunzi wengi kwa Jiji la Dodoma na wanasoma kwa zamu.

"Nini mkakati wa serikali wa kujenga shule katika eneo la Mnada mpya kwa kuwa halina shule kabisa na watoto wengi wanaotoka eneo lile?" alihoji.

Akijibu maswali ya wabunge hao, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, alisema Halmashauri ya Mji wa Tarime imeshatenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya, kuondoa msongamano wa wanafunzi na kuondoa tatizo la wanafunzi kusoma kwa zamu.

"Baadhi ya maeneo tayari wananchi wameanza kujenga shule. Mfano, katika Kata ya Turwa, Chira-Kenyamyori," alisema.

Alisema kutokana na jitihada hizo za wananchi, kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetenga Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya. Itasaidia kuongeza madarasa katika shule za msingi na hivyo kuondokana na msongamano wa wanafunzi darasani. Kuhusu Shule ya Kizota Dodoma, Naibu Waziri huyo alisema serikali kupitia mradi wa BOOST itaangalia namna ya kupata fedha ili kujenga shule nyingine kuondoa adha ya wanafunzi kusoma kwa zamu.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph (kushoto), akibadilishana mkataba na Mwakilishi wa kampuni ya Dohwa Engineering Ltd, Young Joo Oh, baada ya kutiliana saini jijini Dodoma juzi, kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa mradi wa majitaka utakaogharimu Dola za Marekani milioni 70 sawa na Sh. bilioni 164.85. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Hakuna hasara ujenzi wa SGR'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imelieleza Bunge kuwa hakuna hasara yoyote iliyosababishwa na ununuzi wa mkandarasi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Tabora-Kigoma.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhanga Mpina.

Mbunge huyo alihoji lini serikali ilitumia njia ya 'single source' kumpata Mkandarasi CCECC wa Mradi wa SGR LOT 6 Tabora-Kigoma na kusababisha hasara ya Sh. trilioni mbili.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema ununuzi wa mkandarasi ulifuata taratibu zote za ununuzi ikiwamo majadiliano kwa lengo la kuhakikisha gharama sahihi za mradi zinapatikana.

Mwakibete alisema makadirio ya gharama za kihandisi yalikuwa dola za Marekani bilioni 3.066, sawa na Sh. trilioni 7.2 kulinganishwa na gharama halisi za bei ya mkandarasi baada ya majadiliano ambayo ni dola za Marekani bilioni 2.216, sawa na Sh. trilioni 5.2.

"Hii ni baada ya majadiliano yaliyopelekea kuokoa Dola za Marekani milioni 273.91 sawa na Sh. bilioni 632.74 kutoka zabuni ya awali ya Dola za Marekani bilioni 2.49, sawa na Sh. trilioni 5.8.

"Ikumbukwe kuwa utaratibu wa ununuzi kwa njia ya single source ndio uliotumika kumpata Mkandarasi Yapi Merkezi wa ujenzi wa kipande cha 3 (Makutupora-Tabora) na Kipande cha 4 (Tabora-Isaka), ambayo gharama zake ni dola za Marekani bilioni 2.213, sawa na Sh. trilioni 5.19," alisema.

Alibainisha kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma imeainisha njia mbalimbali za ununuzi wa mkandarasi zinazoweza kutumiwa na serikali ikiwa ni pamoja na njia ya single source. "Ununuzi wa mkandarasi kwa kipande cha Tabora-Kigoma ulifuata sheria za ununuzi ambazo ni Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 na kanuni zake namba 161 (1) (a)-(c) za mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016,"alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji kwanini serikali isivunje mkataba wa Shirika la Reli (TRC) na mkandarasi huyo wa ujenzi wa kipande hicho kwa kuwa hata ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2021/22 ilishatahadharisha mkataba huo wa kinyonyaji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema asilimia 65 ujenzi wa SGR unatumia chuma na bei ya soko la dunia imeongezeka. Gharama zinazolinganishwa na mbunge zipo tofauti na hali ya sasa.

"Mkataba hatuwezi kuvunja. Kwanza, ni wa gharama nafuu. Ni mkataba ambao kampuni hii inafanya vizuri kiutendaji duniani," alisema.



# Atiwa mbaroni kwa tuhuma kumpa ujauzito binti yake

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya linamshikilia Musa Pwele (47), mkazi wa Jiji la Mbeya, kwa tuhuma za kufanya mapenzi na mtoto wake na kumpa ujauzito.

Binti huyo (17) ambaye jina lake limehifadhiwa, ni mwanafunzi wa kidato cha pili katika moja ya shule ya sekondari jijini hapa.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Christina Musyani, jana alithibitisha kutokea kwa tukio hilo. Mtuhumiwa alikamatwa Mei 5 mwaka huu baada ya jeshi hilo kupata taarifa kutoka kwa wasamaria wema.

Alidai kuwa Pwele alikamatwa baada ya kumtishia binti yake kuwa hatompatia huduma ikiwamo mahitaji ya shule na huduma nyinginezo. Kutokana na shinikizo hilo alifanikiwa kumnajisi mtoto wake huyo.

Alidai kuwa baada ya binti huyo kutishiwa, alilazimika kumkubalia baba yake ili aendelee kupata mahitaji muhimu na baadaye aligundulika kuwa ni mjamzito.

"Upelelezi wa shauri hilo unaendelea na baada ya kukamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani ili hatua stahiki zichukuliwe na kuwa fundisho kwa watu wengine," alisema Kamanda Christina.

Kamanda Christina alitoa wito kwa wadau wa masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia kuendelea kutoa elimu ili watu wenye tabia hizo waache kuwa zina athari kimwili na kisaikolojia kwa anayetendwa.

Aliongeza kuwa jeshi hilo pia linawataka wadau wa kupinga masuala ya jinsia kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia na kutoa taarifa pindi wanapobaini viashiria vya vitendo hivyo ili hatua za haraka zichukuliwe ikiwamo kuzuia kutendeka kwa ukatili.

Ofisa Ustawi wa Jamii Hospitali ya Igawilo, Habiba Ibrahim alidai binti hiyo alianza kunajisiwa na baba yake akiwa darasa la sita wilayani Sumbawanga.

Alidai kuwa baada ya viongozi kupata taarifa hizo, walimwita Pwele na kumwonya ili aache tabia hiyo lakini walipohamia mkoani Mbeya, aliendelea nayo.

Alidai kuwa baada ya kugundua tukio hilo, uongozi wa Jiji la Mbeya ulimchukua binti huo kwa ajili ya hifadhi mpaka pale atakapojifungua na taratibu nyingine kukamilika.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, ambaye ni Diwani wa Itamboleo, Twalibu Lubandamo (katikati), akizungumza kwenye mkutano wa hadhara na wananchi jamii ya wafugaji kuhusu marufuku ya kuingiza mifugo eneo la Shule ya Msingi Kapunga, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Madiwani wabaini tatizo michezo ya kubahatisha

**Na Grace Mwakalinga,** ILEJE

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Ileje mkoani Songwe limeiomba serikali kupitia upya sheria inayohusu michezo ya kubahatisha kutokana na michezo hiyo kuwa chanzo cha ndoa nyingi kuvunjika na ongezeko la vitendo vya uhalifu.

Diwani wa Viti Maalum, Subira Kyomo, alitoa hoja hiyo juzi wakati wa kikao cha robo ya tatu cha baraza hilo kilichopitia na kujadili taarifa ya mwaka wa fedha 2022/23 kilichofanyika katika ukumbi wa halmashauri hiyo.

Subira alisema michezo ya kubahatisha imekuwa na athari kubwa kwa jamii ikiwapo mmonyoko wa maadili kwa vijana na ongezeko la migogoro katika ndoa.

"Tunapokea malalamiko mengi yanayohusu migogoro ya ndoa hasa kwenye kundi la vijana na sababu kubwa ni hii michezo ya kubahatisha. Mtu hana hata fedha lakini analazimika kuiba au kuharibu bajeti ya familia ili akacheze na unashangaa hata mia hapati," alisema Subira.

Diwani wa Kata ya Itumba, Mohamed Mwala, alisema idadi kubwa ya vijana wanashindwa kujikita katika shughuli za uzalishaji mali kama vile kilimo na badala yake kugeukia mashine za michezo ya kubahatisha.

"Michezo hiyo inapoteza nguvu kazi kwa taifa kwani wengi wao hawashiriki kikamilifu kwenye kilimo au biashara. wanataka fedha za haraka ambazo wakati mwingine hawazipati na kuishia kuliwa tu na hizo mashine," alisema Mwala.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ubatizo Songa, alisema watawasilisha ombi hilo serikalini ili kupitia sheria ya michezo ya kubahatisha ili kuokoa kizazi cha vijana.

# 'Vijana kutoshiriki mikutano ya mitaa ni hatari kwa maendeleo'

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ASILIMIA kubwa ya vijana nchini hawashiriki kabisa mikutano ya mitaa, vijiji na vitongoji kwa ajili ya kujadili shughuli mbalimbali za maendeleo na badala yake kujikita zaidi katika matumizi ya mitandao ya kijamii.

Hali hiyo inatajwa kutowasaidia vijana kutimiza ndoto zao kwa kuwa ushiriki wa vijana katika mikutano ya kujadili masuala mbalimbali ya kijamii kuanzia ngazi ya mtaa una faida ikiwamo kuwa sehemu ya mchakato wa utungaji sheria, uamuzi na kujadili fursa kwa ajili ya manufaa yao.

Mratibu wa mdahalo wa ushiriki wa vijana kwenye masuala ya demokrasia nchini, Hance Njobelo, aliyasema hayo jana wakati wa mdahalo huo ulioandaliwa na Shirika la Empower Youth Prosperity kwa kushirikiana na wadau wengine.

Alisema idadi kubwa ya wanaoshiriki mikutano hiyo ni watu waliozidi miaka 45, hali ambayo inasababisha uamuzi unaofanyika kutomgusa kijana.

"Kuna shida kubwa kwa taifa letu. Ushiriki kwa vijana kwenye mikutano yetu ya vitongoji, mitaa na vijiji ni mdogo. Hali hii inasababisha baadhi ya mambo yanayoamuliwa kutomnufaisha kijana kwa sababu hakuna mtu wa kuwasemea," alisema Njobelo.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Mbeya, Yasin Ngonyani, alisema suala hilo limechangia kwa kiasi kikubwa vijana kutoshirikishwa kwenye ngazi za uamuzi na kusababisha kundi hilo kutokuwa na watu wa kuwasemea kwenye utekelezaji wa sheria mbalimbali.

"Niliwahi kushiriki kwenye mkutano wa kitongoji ambao ulikuwa na lengo la kujadili maendeleo ya eneo letu ikiwamo ujenzi wa soko na kudhibiti mauaji. Kwa bahati mbaya, mimi pekee ndiye kijana niliyehudhuria. Hali hii inaonyesha ni kwa namna gani vijana hawatambui umuhimu wa kushiriki mikutano ya namna hii.

"Mikutano hii ni sehemu ya fursa kwa vijana kwa ajili ya kuandaa sheria na mahitaji yao vilevile kuandaliwa kuwa viongozi wazuri hapo baadaye kwa sababu ngazi ya mitaa na vitongozi ni muhimu kwa ajili ya uamuzi wowote wa maendeleo," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Empower Youth Prosperity (EYP) Ipyana Mwakyusa, alisema lengo la kuandaa mdahalo wa demokrasia kwa vijana ni kujadili na kuchochea maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko na kulijenga taifa.

Mwakyusa alisema zaidi ya vijana 100 wa kada mbalimbali toka mkoani Mbeya, wameshiriki mdahalo huo ambao wamejadili kwa namna gani demokrasia inatoa nafasi kwao kushiriki kikamilifu kwenye maendeleo ya taifa.

"Kwa kutambua vikwazo vitokanavyo na demokrasia wanazopitia vijana, mdahalo huu utatusaidia kuandaa mkakati na mwelekeo wa kulenga uimarishaji wa ushiriki wa watu wote kwenye masuala ya utawala na sheria kupitia falsafa ya 4R yaani maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko kujenga upya," alieleza.

Akifungua mdahalo huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka vijana kuwa wazalendo, wabunifu, wachapa kazi na kutunza heshima yao ili kutengeneza kesho yao iliyo bora zaidi badala ya kuwa wafuasi wa wanasiasa ambao baadhi wanawatumia kwa maslahi yao. Aliwataka vijana kutumia vyema fursa zilizotolewa na Wizara ya Kilimo kupitia programu ya kujenga kesho iliyo bora ambyo kwa Mkoa wa Mbeya kuna zaidi ya ekari 50 zimetengwa wilayani Chunya kwa ajili ya kilimo cha ufuta.

Alisema fursa hiyo ni bure kwa vijana - kila kijana anakaribishwa kuwekeza kwenye kilimo cha ufuta ili kujikwamua kiuchumi na kuwahakikishia soko la uhakika la bidhaa hiyo.

"Vijana ninawashauri mjikite zaidi kwenye kufanya kazi kwa bidii ili mmiliki uchumi wenu binafsi, hao wanasiasa mnaotamani kupiga nao picha kisha mnaposti kwenye mitandao ya kijamii haiwasaidii chochote. Muda huo utumieni kutafuta fursa za kumiliki uchumi kupitia nyanja mbalimbali," alisema Homera.

Aliipongeza serikali kwa kuboresha maridhiano nchini na kujenga uhusiano mzuri baina ya vyama vya siasa na wanasiasa kuliko ilivyokuwa awali.

Katibu wa Baraza la Vijana wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA) Mkoa wa Mbeya, Emily Mwakilembe, alisema ili kuboresha maridhiano nchini, ni vyema wanasiasa waliokosana, kuombana msamaha hadharani kama sehemu ya maridhiano nchini.



# Utalii kupaisha uchumi wa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UCHUMI wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.1 mwaka huu kutokana na kuongezeka kwa asilimia 30 ya uingiaji wa watalii watakaotembelea visiwa.

Ongezeko hilo ni kutoka watalii 548,503 kwa mwaka 2022 hadi watalii 713,053 mwaka 2023.

Hayo yamesemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, nje ya mji wa Zanzibar na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka 2023/2024.

Hemed alitaja sababu zingine ni kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwamo miundombinu ya barabara za mjini na vijijini, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, Bandari ya Mangapwani na ukarabati wa Bandari ya Malindi, Unguja. Alisema miradi mingine itakayochangia ukuaji wa uchumi ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii kama vile afya, elimu, majisafi na salama na ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila wilaya.

"Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili kubakia kwa tarakimu moja, kuongezeka kwa usimamizi wa ukusanyaji wa mapato na matumizi ya serikali, kuongezeka kwa hatua za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza miradi binafsi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje na serikali kuongeza usimamizi wa miradi ya kimkakati," alisema.

Kuhusu maendeleo ya uwekezaji, Hemed alisema serikali imesajili miradi ya uwekezaji 60 hadi kufikia Machi, mwaka huu, ambayo inatengeneza mtaji wa makisio ya Dola 433,077,054 na inatarajiwa kutengeneza ajira 1,937.

Pia alisema katika mwelekeo wa bajeti mpya, serikali imepanga pamoja na mambo mingine, kupokea na kusajili miradi 100 ambayo itatengeneza mtaji wa Dola milioni 15,500 na kutengeneza ajira 2,000.

Kadhalika, alisema kilimo bado kinaendelea kuwa ni tegemeo la wananchi wengi katika kujikimu maisha yao na serikali inaendelea kuchukua kila aina ya jitihada za kuiinua na kuimarisha sekta hiyo. Mojawapo ya mikakati, alisema ni kuwaendeleza wakulima kulima kitaalamu zaidi ili wapate mazao mengi na yaliyo katika hali ya ubora kwa ajili ya chakula na biashara. Alisema kumekuwa na ongezeko la usafirishaji wa mazao ya biashara na kwamba tani 4,681.5 za karafuu zenye thamani ya Sh. bilioni 3.5 mwaka 2022 zilisafirishwa na mwani tani 23,158 zenye thamani Sh. bilioni 50.5 mwaka 2022 na mazao mingine ya baharini tani 11,743.7 zenye thamani ya Sh. bilioni 28.4.

Alisema pato la taifa kwa mwaka 2022, limeongezeka kutoka Sh. trilioni 3.275 mwaka 2021 na kufikia Sh. trilioni 3.498.

Kuhusu kasi ya mfumuko wa bei kwa mwaka 2022, alisema imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 5.1 kutoka wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2021. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa bei ya bidhaa zote za chakula na zisizo za chakula.

"Kasi hii ya mfumuko wa bei bado imeendelea kuleta changamoto katika uchumi wetu na katika upatikanaji wa bidhaa kwa wananchi. Serikali inaendelea kuchukua hatua ili kudhibiti mfumuko huu," alisema.

Hemed aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha Sh. 75,316,057,026 kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwa ofisi yake na taasisi zake kwa ajili ya kutekeleza programu mbalimbali za maendeleo.



Balozi wa Ufalme wa Uholanzi nchini Tanzania, Wiebe de Boer na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, wakionyesha hati za makubaliano ya ushirikiano wa kuimarisha vyeti vya kielektroniki (E-cert), kwa ajili ya mazingira na kilimo cha bustani za mboga nchini, baada ya kutiliana saini mjini Dodoma jana. Wengine ni Mshauri wa Kilimo wa Uholanzi nchini Kenya na Tanzania, Bart Pauwels (kulia) na Ofisa kutoka Wizara ya Kilimo, Ellen Rwijage. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# SMZ yaweka sawa taarifa upotevu fedha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Fedha na Mipango Zanzibar imesema si kweli kwamba kuna upotevu mkubwa wa fedha za serikali kupitia mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Ali Suleiman Ameir, amesema lengo la serikali la kuimarisha mifumo ni kudhibiti upotevu wa fedha uliokuwa ukitokea katika miaka ya nyuma.

Ameir alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi la Wawi, Bakari Hamad, aliyetaka kujua ni upi mkakati wa serikali katika kudhibiti fedha za wananchi kuendelea kupotea kutokana na upotevu kupitia mfumo huo.

Alisema matumizi ya mifumo yamesaidia kuimarisha mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kadri siku zinavyoendelea kupitia taasisi zilizopewa dhamana ya ukusanyaji mapato.

Katika kipindi cha miezi tisa, alisema Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), imekusanya Sh. bilioni 449.283 sawa na asilimia 97.56 ya makadirio ya makusanyo ya Sh. bilioni 460.499.

"Makusanyo haya ni ongezeko la Sh. bilioni 274.799 sawa na ukuaji wa asilimia 63.50 ya kipindi cha miezi tisa kwa mwaka 2021/2022. Kwa upande wa TRA, makusanyo yameongezeka kwa asilimia 27 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka 2021/22," alisema.

Pia alisema mapato yasiyo kuwa ya kodi yamefikia Sh. bilioni 67.296 na serikali katika udhibiti zaidi wa upotevu wa mapato, imejiwekea mikakati ya kuanzishwa na kuimarisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani za Serikali.

# Serikali yakwazwa matuta barabarani

**Na Rahma Suleiman,**
ZAZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imeelezea kuchukizwa na hatua za baadhi ya wananchi za kuweka matuta katika barabara jambo ambalo ni kinyume cha Sheria ya Barabara kifungu cha 18.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Nadil Abdulatif, alisema wizara hiyo inaendelea kufuatilia kwa kufanya ukaguzi na usafi wa barabra kila mwezi ili kubaini uharibifu wa njia na kasoro zinazojitokeza na hatimaye kuchukua hatua stahiki.

Abdulatif alisema hayo jana katika wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Tumbe, Said Saleh Salum, aliyetaka kujua hatua zinazochukuliwa za uwekaji wa matuta kiholela katika barabara katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Naibu Waziri alisema kwa mujibu wa marekebisho ya Sheria ya Barabara kifungu cha 18 ni kosa na haikubaliki kwa mwananchi yeyote kufanya au kuweka kitu chochote kwenye barabara na pembezoni mwa maeneo ya barabara.

"Mheshimiwa Spika, kifungu 18 (2) cha Sheria ya Barabara kinaeleza hatua zinazopaswa kuchukuliwa lakini kwa sasa hatua tunazozichukua ni kuyaondosha matuta ambayo yamewekwa kinyume cha utaratibu wa Wakalawa Barabara," alisema.

Alisema kazi hiyo inafanyika kwa kushirikiana na ofisi za mikoa na wilaya pamoja na halmashauri na mabaraza ya miji na vyombo vya ulinzi na usalama likiwamo Jeshi la Polisi.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakiweka matuta barabarani kama kizuizi cha ajali za barabani ili magari yasitembee kwa mwendokasi hasa katika maeneo ambayo yana harakati nyingi.

"Tutahakikisha tunawachukulia hatua wananchi wote ambao wataweka matuta barabarani bila ya kufuata sheria," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 45 of 2023**
**In the matter of the late AUGUSTINE SALIELI NGOWI of Image, within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by ADELFRIDA YASINI MTUI**
**PETITION FOR LETTER OF ADMINISTRATION WHEN THE DECEASED DIED INTESTATE (SECTION 56)**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 1 day of 6......., 2023
Dated at Dodoma this 10 day of 5..........., 2023

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MWAROGO SHUARI HAMISI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Suzuki ESCUDO yenye namba za usajili T 170 AJP, Chassis No. TAOIW849687, Engine No. G16A271932. Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/463505/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER FELEX MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye usajili namba: **T 139 CTC , CHASSIS NAMBA: FS418U550231** na **ENGINE NAMBA: 6D220231**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/161045/2023**

**THE REGISTRATIONS OF DOCUMENT ACT (CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDRPOLL**
**BY THIS DEED**

**KULWA ATHUMANI MAKOMBORA** of **P.O.BOX 166**, Morogoro formerly knows as , do hereby absoltely renounce and abundon the use of my former name **ALLY ATHUMAN MAKOMBOLA** and in lieu thereof to assume as from date before of the name of **KULWA ATHUMANI MAKOMBORA.**
**AND IN PURSUANCE** of such change of names as aforesaid , I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records deed and instruments in writting and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions whatsoever use and sign the said name of **KUILWA ATHUMANI MAKOMBORA** as my name to lieu of the former name of **ALLY ATHUMANI MAKOMBORA** as renouced, due to all transactions records, transcript and certificate I prefer to use the name of **KULWA ATHUMANI MAKOMBORA.**
**AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUEST** all persons to designate and address me by of **KULWA ATHUMANI MAKOMBORA** only.
The reason to change name is that the name **ALLY AATHUMANI MAKOMBORA** has been used mistakenly on recording my details from the beginning by writting another person's name instead of mine in my National Identity card No. **19891003-67226-00001-27**, while the name **KULWA ATHUMANI MAKOMBORA** used in my **NSSF** Identify card as the biological father. I wish to be identofied by my real names **KULWA ATHUMANI MAKOMBORA** to be identified.
I the said **KULWA ATHUMANI MAKOMBORA** make this declaration conscientiously believing the same to be true in accordance with the provisions of the Oaths (Judical Proceedings) and statutory Declaration Act, 1966.
**IN WITNESS S WHEREOF** I have excuted this Deed this 09th day of May 2023.



*OFISI ZA MATANGAZO*
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*

AMBUYANA. T.F.S. DEBT COLLECTOR AND AUCTIONEER COMPANY LTD

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

| MDAIWA | DALALI | AINA YA DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| ALISON.E .AKYOO | **AMBUYANA .T .F .S AUCTIONEER** | NYUMBA(PAGA LE)iliyopo kijiji cha SHABAHA MOSHI VIJIJINI | 19/05/2023 |
| CHRISTO PHER. E .KAKAI | **AMBUYANA .T. F .S AUCTIONEER** | NYUMBA iliyopo kindi/miembeni Moshi Vijijini | 25/05.2023 |

**Masharti ya Mnada:**
Mnada utafanyika Mahali Dhamana iliyopo kuanzia saa tatu Asubuhi Mteja atalipa 25% Siku ya Mnada 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% Hairudishwi.Gharama za kubadili umiliki ni juu ya Mnunuzi

**Mawasiliano piga**
**0746-063366/0752-605575**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA



Ofisa Rasilimali Watu wa Kampuni ya Barrick North Mara, Gema Salamba, akizungumza na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe mkoani Morogoro, wakati wa kongamano la kuwajengea uwezo wa kuibua vipaji na kuchangamkia fursa lililoandaliwa na Taasisi ya AIESEC na kufanyika juzi kwa udhamini wa kampuni hiyo.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni ya GGML kukusanya bilioni 2/- za kudhibiti UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI ya GGML Kili Challenge inayoratibiwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), mwaka huu inatarajiwa kukusanya dola za Marekani milioni moja, sawa na Sh. bilioni 2.3.

Fedha hizo ambazo hukusanywa kila mwaka, hulenga kuchangia juhudi za serikali kufikia malengo ya sifuri tatu, yaani kupunguza kabisa kwa kufikia asilimia sifuri ya maambukizi mapya, sifuri ya unyanyapaa na sifuri katika vifo vitokanavyo na UKIMWI.

Hayo yalibainishwa jana mjini Moshi mkoani Kilimanjaro na Makamu Rais wa AngloGold Ashanti- GGML anayesimamia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo, wakati wa hafla ya uzinduzi wa harambee ya uchangiaji wa fedha hizo kupitia kampeni hiyo ya GGML Kili Challenge kwa mwaka 2023.

Mbali na kuishukuru serikali kwa kuunga mkono kampeni hiyo iliyoasisiwa mwaka 2002, Shayo alisema wakiwa wadau wa mapambano hayo ya UKIMWI na VVU, GGML imepokea msaada ambao uliiwezesha Kili Challenge kupiga hatua kubwa hadi kufikia kuwa mfuko wa kimataifa, wenye kushirikisha wapanda mlima na waendesha baiskeli kutoka mabara yote na zaidi ya nchi 20.

"Mwaka huu tumekuja tena kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, hivyo GGM kwa kushirikiana na TACAIDS tunawakaribisha sana wadau wetu na kampuni mbalimbali kuchangia na kushiriki kampeni hii.

"Kipekee tunapenda kutambua ushirikiano wa baadhi ya kampuni na taasisi mbalimbali ambazo tayari zimeshajitokeza kuchangia mfuko katika mwaka huu wa 2023. Nina imani wadau waliojitokeza leo watatusaidia kwa kiasi kikubwa kufikia malengo ya kukusanya milioni 250," alisema.

Aliongeza kuwa VVU/UKIMWI bado ni tatizo kubwa nchini kwa kuwa takwimu za maambukizi mapya ya VVU haziridhishi, hususani kwa makundi maalum wakiwamo vijana.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alizipongeza GGML na TACAIDS kwa kuendelea kuutumia Mlima Kilimanjaro kama kivutio kinachotumika kukusanya fedha kwa ajili ya mwitikio wa VVU na UKIMWI.

Alisema jambo hilo limechangia kwa kiasi kikubwa katika kuutangaza mlima huo maarufu duniani na hivyo kuongeza idadi ya watalii.

"Ninakaribisha mawazo, ushauri kutoka kwenu na wadau wengine wa jinsi ya kuboresha zaidi kampeni hii. Ninatoa wito kwa watu binafsi, mashirika, taasisi na kampuni nyingine kuiga mfano wa GGML kwa kujitoa zaidi kuchangia rasilimali za mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini, hususan katika kipindi hiki ambapo michango ya wahisani kutoka nje ya nchi inaendelea kupungua kwa sababu mbalimbali," alisema.

Kupanda mlima kunatarajiwa kuanza Julai 14 na kushuka Julai 20 mwaka huu.

## TRA yatoa mafunzo kwa wamiliki na watumiaji maeneo ya kuhifadhi bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetoa mafunzo kwa wamiliki na watumiaji wa maeneo ya kuhifadhi bidhaa mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza na wadau wa walioshiriki semina hiyo jijini jana, Kamishna wa Kodi za Ndani, Herbert Kabyemela aliwakumbusha wamiliki na watumiaji wa maghala ya kuhifadhi bidhaa ( Storage Facilities) kusajili maghala yao kwa Kamishna Mkuu wa TRA kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa kodi.

Mwezeshaji wa semina hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Elimu na Huduma kwa Mlipakodi, Stephen Kauzeni, alifafanua kiundani Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 kifungu cha 45A, kwamba kinawataka wamiliki (au watumiaji) wa maeneo ya kuhifadhi bidhaa, kusajili maeneo hayo kwa Kamishna Mkuu.

Wafanyabiashara waliishukuru na kuipongeza TRA kwa semina hiyo kwa kuwa baadhi walikuwa hawana uelewa kuhusu mabadiliko hayo ya sheria na kushindwa kutimiza wajibu wao wa kusajili maeneo yao ya kuhifadhia bidhaa kwa wakati.

TRA kupitia Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi imekuwa ikiendesha semina mbalimbali kuhusu masuala mbalimbali ya kikodi ili kuwajengea uelewa walipakodi.

Ijumaa iliyopita, TRA ilitoa tangazo la kuwakumbusha wamiliki na watumiaji wa maeneo ya kuhifadhia bidhaa za umma kwamba Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022, Kifungu cha 45A chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438, kinawataka wamiliki na watumiaji wa maeneo ya kuhifadhi bidhaa kusajili maeneo hayo kwa Kamishna Mkuu. Kifungu hicho kilianza kutumika rasmi Julai 2022.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed






Washindi wa Shindano la Parimatch VIP Experience wakiwa katika picha ya pamoja na mabalozi wa kampuni hiyo. Kushoto ni Masatu Amon Ndaro na kulia ni Sultan Omary 'Sullboe'. **MPIGAPICHA WETU**

# Parimatch yapeleka Wananchi nusu fainali

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubashiri ya Parimatch imetoa zawadi za tiketi za VIP A pamoja na jezi kwa washindi kutoka kwenye kampeni yao ya 'Parimatch VIP Experience' ambao ni wapenzi wa mchezo wa soka na mashabiki wa timu kongwe ya Yanga, kwenda kushuhudia mtanange wa nusu fainali ya mkondo wa kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants FC ya Afrika Kusini, uliochezwa jana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga ilitinga hatua hiyo baada ya kuitoa Rivers United kwa jumla ya mabao 2-0 ambayo waliyapata kwenye mchezo wa kwanza nchini Nigeria kabla ya kutoka suluhu kwa Mkapa Aprili 30, mwaka huu.

Aidha, Afisa Habari na Mawasiliano kwa Umma wa Parimatch Tanzania, Ismael Mohamed, amewataja washindi hao kuwa ni Bahati Mbatta, Benedicto Yona, Gerald Mathias, Fred Bryan pamoja na Baraka Kimaro ambao wote wametokea maeneo tofauti ya jijini Dar es Salaam.

Pia, afisa habari huyo ameonesha kufarihishwa kwa ushindi wa Bahati, ambaye amekuwa mshindi wa kwanza kwa wanawake kujishindia tiketi na jezi tangu kuanza kwa mashindano hayo.

"Ushindi wa Bahati unaonesha kuwa sasa michezo ya kubashiri inazidi kushika kasi na inazidi kukubalika katika jamii, hii ni motisha kwa wanawake na mabinti wote ambao walidhani michezo hii ni kwa ajili ya wanaume tu.

"Parimatch Tanzania wametoa fursa hii kwa Watanzania wote, haijalishi jinsia, kama una umri wa miaka 18 na kuendelea jukwaa ni lako kujaribu bahati yako leo. Tembelea www.parimatch.co.tz ufungue akaunti yako kama hujajiunga ili uwe wa kwanza kuburudika na kufaidika nasi kwani kuna mambo mengi mazuri yanakuja siku za hivi karibuni," alisema Ismael.

Kwa upande wa mashabiki hao kwa ujumla wamelisema wamejisikia furaha kuona Parimatch imewawekea historia katika maisha yako kwa kuweza kushuhudia mtanange wa nusu fainali ya kwanza nchini kati ya Yanga na Marumo ikipigwa katika Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam.

Kampuni ya Parimatch ndio kinara wa michezo ya kubashiri mtandaoni na imekuwa ikitoa ofa kubwa ya bonasi ya Ukaribisho ya asilimia 100 hadi kufikia Sh. milioni moja kwa wateja wapya wanaojiunga nao.

# MECHI JKT QUEENS, FOUNTAIN GATE KUAMUA UBINGWA SIMBA QUEENS

**Na Adam Fungamwango**

HATMA ya Simba Queens kutwaa tena kwa mara ya nne ubingwa wa Tanzania Bara kwa Soka la Wanawake huenda ikajulikana leo wakati JKT Queens itakapokuwa ugenini kuikabili Fountain Gate Princess katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Simba Queens ambayo juzi ilipata ushindi wa mabao 2-0 kwenye uwanja huo huo dhidi ya Baobab Queens, itakuwa ikiombea mechi ya leo imalizike kwa sare au ushindi uende kwa Fountain Gate Princess ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kutwaa ubingwa huo.

**Mabao ya juzi ya Simba Queens yalifungwa na Jentrix Shikangwa, straika hatari kutoka Kenya aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo, ambaye ametimiza jumla ya mabao 16, akiongoza kwenye jedwali la ufungaji, Mrundi Joelle Bukuru akiongeza la pili dakika za mwisho wa mchezo.**

Ni matokeo yaliyoipeleka tena kileleni na pointi 42, ikiwa imebakisha mechi moja tu dhidi ya Ceasiaa Queens utakaochezwa kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Mkwawa Mei 17, mwaka huu.

JKT Queens ina pointi 40, ambapo kama ikishinda zote itafikisha alama 46 na kutwaa umalkia, huku Simba Queens ikimaliza na pointi 45, hivyo sare yoyote au kufungwa ni ahueni kubwa kwa mabingwa hao.

Fountaina Gate Princess nayo ina nafasi ya kutwaa ubingwa kama itashinda mechi ya leo, kwani kwa pointi 38 ilizonazo kama itashinda leo itafikisha alama 41, na mechi ya mwisho ikipata matokeo mazuri itamaliza na pointi 44, huku ikiziombea mabaya timu za Simba Queens na JKT Queens zipoteze michezo yao.

Awali mechi hiyo ilikuwa uchezwe jana, lakini Afisa Mtendaji Mkuu wa Fountain Gate, Augustine Ngamesha alisema wamepata maagizo kutoka Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuwa mechi hiyo ipelekwe mbele kwa siku moja kupisha mechi ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kati ya Yanga na Marumo Gallants iliyochezwa jana Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# Meridianbet, Awesu warudisha fadhila kwa jamii

**Na Saada Akida**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubashiri ya Meridianbet Tanzania, kwa kushirikiana na kiungo wa timu ya KMC FC, Awesu Awesu, wametoa zawadi kwa watu wasiojiweza zenye thamani ya Sh. milioni moja katika mtaa wa Magomeni, alikozaliwa na kukulia mchezaji huyo.

Mbali na fedha hizo pia wametoa mafuta ya kupikia, sukari, mchele, sabuni na vifaa vya kufanyia usafi pamoja na kutembelea Shule ya Msingi Magomeni kwa ajili ya kuwahamasisha wanafunzi kucheza soka ambapo walitoa zoezi la kupiga penalti tano na kuwapa washindi zawadi.

Akizungumza na Nipashe jana, Awesu alisema anamshukuru Mungu kumwezesha kufika katika mtaa huo kwa kushirikiana na Meridianbet kutoa msaada kwa watu ambao hawajiwezi na kwenda kutembelea shule kwa ajili ya kuhamasisha michezo shuleni.

"Ni jambo la kujivunia kurudisha shukrani mtaani kwangu hasa kuwakumbuka wasiojiweza, lakini kubwa zaidi nawashukuru wadhamini wetu Meridianbet kuwaunga wachezaji kuwafikia na kuwafariji wale wasiojiweza.

"Leo nimefanikiwa kufika hapa mtaani kwangu kutoa msaada kwa jamii yangu iliyonikuza na kunilea, nawashukuru sana Meridianbet namna wanavyohakikisha wanarudisha kwa jamii hata kile kidogo tunachokipata," alisema kiungo huyo wa KMC FC.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na masoko kutoka Meridianbet, Matina Nkurlu, alisema kilichofanywa na kiungo huyo ni uungwana kwa maana ya tafsiri ya uungwana ni pamoja na kujali njia alizopita na kuzipa furaha.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RAMOS ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imefanya mazungumzo na Benfica kuhusu mkataba wenye thamani ya hadi pauni milioni 100, ikijumuisha nyongeza, kwa ajili ya mshambuliaji wa Ureno, Goncalo Ramos, mwenye umri wa miaka 21. ***(Mirror)***

### KANTE KUBAKIZWA CHELSEA

CHELSEA inatumaini kuwa uteuzi wa Mauricio Pochettino kama kocha unaweza kumshawishi kiungo wa Ufaransa, N'Golo Kante, mwenye umri wa miaka 32, kusaini mkataba mpya Stamford Bridge. ***(Telegraph)***

### AUBAMEYANG KUTOLEWA

CHELSEA iko tayari kumtoa mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, mwenye umri wa miaka 33, na mlinzi wa Hispania, Marc Cucurella mwenye miaka 24, katika mpango wa kubadilisha mkopo wa mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix (23), kutoka Atletico Madrid kuwa mkataba wa kudumu. ***(Standard)***

### RICE AGOMBEWA EPL

KLABU ya Manchester United iko tayari kumenyana na Arsenal na Chelsea kwa ajili ya kuinasa saini ya Declan Rice baada ya kufurahishwa na kiwango cha kiungo huyo wa England mwenye umri wa miaka 24, akiwa na West Ham dhidi ya 'Mashetani Wekundu' hao Jumapili. ***(Sun)***

### GYOKERES AIVUTIA WEST HAM

WEST Ham inavutiwa na mshambuliaji wa Coventry City mwenye umri wa miaka 24, Viktor Gyokeres. ***(Mirror)***

### AWANIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinazotarajiwa kupambana na Inter Milan na Juventus kuwania saini ya beki wa Monza, Mbrazil Carlos Augusto, 24. ***(Clciomercato)***

### SCHMADTKE ATAKIWA

LIVERPOOL ipo kwenye mazungumzo juu ya kumteua Mjerumani Jorg Schmadtke kuwa mkurugenzi wao mpya wa michezo. ***(Mail)***

### FULHAM YAMTAKA SILVA

KOCHA wa Fulham, Marco Silva, ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni sita kwenye mkataba wake, huku West Ham, ikionesha nia ya kumtaka Mreno huyo mwenye umri wa miaka 45, iwapo wataamua kumfuta kazi David Moyes mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

### DE GEA AKUBALI UNITED

DAVID de Gea amekubali kusaini mkataba mpya na Manchester United kwa masharti yaliyopunguzwa, lakini hakuna uhakika kwamba mlinda mlango huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 32, atakuwa namba moja wa klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### ISMAEL KUTUA WATFORD

KOCHA wa zamani wa West Brom na Barnsley, Valerien Ismael, amepiga hatu katika mazungumzo ya kuwa kocha wa Watford. ***(Athletic)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SAKA AKUBALI KUTIA SAINI MKATABA MPYA ARSENAL

**●●● Inaaminika kuwa picha za matangazo zitakazotolewa pamoja na tangazo hilo...**

**LONDON,** England

ARSENAL inatarajia kutangaza mkataba mpya wa Bukayo Saka kabla ya mwisho wa msimu wa Ligi Kuu ya England 2022/23.

**Fowadi huyo wa England amekuwa kwenye mazungumzo na klabu hiyo tangu mwaka jana, na sasa amekubali kutia saini mkataba mpya wakati wa majira ya joto.**

Saka mwenye umri wa miaka 21, amekuwa na jukumu muhimu katika changamoto ya ubingwa wa 'Washikabunduki' hao msimu huu.

Amefunga mabao 13 na kutoa pasi za mabao 11 kuwasaidia vijana hao wa kocha Mikel Arteta kushika nafasi ya pili na kusalia katika kuwinda taji kuelekea wiki za mwisho za msimu huu.

Saka amekosa saa moja tu ya kucheza ligi msimu huu na pia alifunga mabao matatu kwenye Kombe la Dunia huku England ikifuzu robo fainali kule nchini Qatar.

Mazungumzo na Arsenal kuhusu masharti mapya yameanzia msimu uliopita wa majira ya joto, huku Agosti mwaka huu, Saka akisema "nilishiriki kwa imani" na Arteta kwamba angeongeza mkataba wake katika Uwanja wa Emirates.

Shirika la Habari la PA linaelewa kuwa makubaliano yamefikiwa kwa mkataba mpya ambapo wa sasa ulitiwa saini msimu wa majira ya joto wa 2020 na unamalizika mwaka ujao.

Inaaminika kuwa picha za matangazo zitakazotolewa pamoja na tangazo hilo tayari zimekamilika na ni suala au kufanyiwa kazi kwa maelezo zaidi kabla ya mkataba kukamilika.

Wakati Saka anakaribia kuweka mustakabali wake wa muda mrefu na Arsenal, Granit Xhaka anaweza kuhama msimu huu wa majira ya joto.

Inafahamika kuwa klabu hiyo itakuwa tayari kumwachia nahodha huyo wa Uswisi, ambaye mkataba wake pia unamalizika mwaka 2024, aende ikiwa watapata ofa wanayoona inakubalika.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,112,4
MECHI KALI
JUVENTUS
VERSUS
SEVILLA FC
1 | 1.82
X | 3.25
2 | 4.46
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANCELOTTI AKATAA BAO LA DE BRUYNE



**MANCHESTER,** England

CARLO Ancelotti alimkosoa mwamuzi, Artur Soares Dias, baada ya Real Madrid kutoka sare ya 1-1 na Manchester City katika mchezo wao wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne, akisema bao la kusawazisha la City halikuwa halali.

Kevin De Bruyne aliisawazishia City dakika ya 67 kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu - baada ya Vinicius Junior kuiweka Madrid mbele kwa bao zuri kipindi cha kwanza - na kabla ya mechi ya mkondo wa pili katika Uwanja wa Etihad, Mei 17, mwaka huu.


Kocha huyo raia wa Italia alisema ameona picha za runinga ambazo zilionesha mpira haukuchezwa kwenye mstari wa karibu na kugusa, sekunde chache kabla ya bao la De Bruyne.

"Ilionekana kama mpira ulikuwa nje," alisema Ancelotti akiiambia Movistar.

"Na kabla ya hapo, kulikuwa na kona ambayo mwamuzi hakutoa. Mwamuzi hakuwa makini sana. Alinipa kadi ya njano, na nikasema, 'Wape uwanjani, si nje!' "Ulikuwa umetoka. Si mimi nasema hivyo; teknolojia ndivyo inavyosema," aliongeza Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Inanishangaza. Ni maelezo madogo, lakini mwamuzi hakuwa makini. Wachezaji walistahili kadi nyingi zaidi uwanjani, si mimi nje ya uwanja."

Mechi hiyo ni marudio ya Nusu Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya mwaka jana, ambayo ilishuhudiwa Madrid ikisonga mbele kwa jumla ya mabao 6-5 baada ya kuibuka na ushindi wa 3-1 katika mchezo wa marudiano uliochezwa Bernabeu.



# *Baba akanusha Messi kuhamia Saudi Arabia*

**PARIS,** Ufaransa

BABA na wakala wa Lionel Messi, Jorge, amekanusha ripoti kwamba mshambuliaji huyo ana makubaliano ya kuhamia Saudi Arabia msimu ujao wakati mkataba wake na Paris Saint-Germain utakapomalizika.

"Hakuna chochote kinachofaa na klabu yoyote kwa msimu ujao," alisema katika taarifa Jumanne.

"Uamuzi hautawahi kuchukuliwa kabla ya Lionel kumaliza kampeni ya ligi na PSG.

"Mara tu msimu unapomalizika, huo utakuwa wakati wa kuchambua mambo na kuona chaguzi zipi na kuchukua uamuzi.

"Siku zote kuna uvumi na wengi hutumia jina la Lionel, lakini kuna ukweli mmoja tu na ni kwamba tunaweza kuhakikisha kuwa hakuna chochote kilichokubaliwa na mtu yeyote. Si kwa maneno, si saini, hakuna makubaliano. Na hakutakuwa na chochote..

Messi mwenye umri wa miaka 35, mkataba wake
unamalizika Juni, na mu
takabali wake bado hauj
likani. Vyanzo viliiamb
ESPN wiki iliyopita kwar
ba ataondoka PSG baac
ya miaka miwili nchi
Ufaransa, lakini hatua yal
inayofuata bado haij
likani.

Wakati mjadala w
kwenda Saudi Arab
haujafungwa, vyanzo vi
iambia ESPN hapo awa
kwamba Messi anafikir
kuhamia Al Hilal, wa
inzani wa timu ya Al Nas
anayocheza Cristiano Ro
aldo.

62,859/-



# YANGA, UNICEF NA SERIKALI ZATOA ELIMU KIPINDUPINDU

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU kongwe nchini, Yanga kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (Unicef), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kupitia Ofisi ya Afya ya Mkoa wameungana pamoja kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa mlipuko wa kipindupindu.

**Tukio hilo la kutoa elimu lilifanyika jana asubuhi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakati timu hiyo, ikijiandaa na mchezo wa mkondo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini.**

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andre Mtine, alisema elimu hiyo imetolewa kwa mashabiki wote waliofika uwanjani hapo, na kwamba kikubwa wametakiwa kuchukua hatua katika kuelekeza kuongeza uelewa endelevu kuhusu kuzuia na kudhibiti magonjwa yote yanayosambazwa kwa njia ya maji yanayosababishwa na aina ya vijidudu ikiwa ni pamoja na mlipuko wa kipindupindu.

Mtine alizitaja hatua zitakazochukuliwa na Yanga kuwa ya kwanza ni upatikanaji na matumizi ya majisafi ya kunywa kwa kuchemsha na kutibu maji kwa klorini. Pili kushughulikia hali duni ya usafi wa mazingira na usafi binafsi, hiyo ikijumuisha kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya vyoo/majiko, uondoaji wa taka za maji na taka za viwandani, kuboresha usafi binafsi na usalama sahihi wa chakula.

Alisema mpango huo utakuwa endelevu na utajumuisha shughuli mbalimbali kama programu za kufikia jamii, kampeni za kuongeza uelewa wa umma, na vifaa vya elimu kama vile vipeperushi na matangazo ya redio.

"Tunafurahi kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika kampeni muhimu hii ya kuongeza uelewa juu ya magonjwa yote ya kuharisha ikiwa ni pamoja na mlipuko wa kipindupindu. Kama klabu ya michezo, tumeweka azimio la kukuza afya na ustawi wa mashabiki na jamii yetu, kama tulivyodhihirisha hapo awali wakati tulipoanza kampeni yetu kwa ajili ya chanjo ya COVID-19," alisema.

Akishiriki katika juhudi hizo, Daktari Rashid Mfaume, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema: "Ushirikiano na Yanga ni mfano wa jinsi ushirikiano kati ya wadau tofauti unavyoweza kucheza jukumu muhimu katika kukabiliana na changamoto za afya ya umma.

"Tunafurahi kushirikiana na Yanga tena, katika kuongeza uelewa na elimu kwa umma hata baada ya kumalizika kwa mlipuko wa kipindupindu.

"Nawaomba sana mashabiki wa Yanga na jamii kwa ujumla kushiriki kwa hiari katika shughuli za jamii zinazokuja ili kumaliza sababu zote za magonjwa yanayoambukizwa na maji, kuboresha afya na usafi wa mazingira, kuboresha usafi wa kibinafsi na matumizi ya maji salama ya kunywa.

"Mwisho lakini si kwa umuhimu mdogo, ni ruhusu tena kuwasilisha shukrani zangu za dhati kwa UNICEF, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Yanga Sports Club," alisema.




Mashabiki wa Yanga, wakipata elimu ya namna ya kujikinga na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu katika kampeni inayoendeshwa na klabu hiyo kwa ushirikiano na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (Unicef) na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kupitia Ofisi ya Afya ya Mkoa. Kampeni hiyo ilifanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana kabla ya mechi ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba njia nyeupe kwa Yahya Mbegu

INATOKA UK. 23

Kwa upande wa Mtendaji Mkuu wa Simba, Kajula akizungumza na Nipashe jana, alisema wamejipanga kufanya usajili mkubwa baada ya kushindwa kufanya vizuri msimu huu kwa lengo la kuboresha kikosi hicho kinachotarajia kushiriki michuano ya Super League.

"Akili na nguvu zetu ni kuboresha kikosi kwa ajili ya Super League, Simba ni miongoni timu nane katika Bara la Afrika itakayoshiriki michuano hiyo, lazima tufanye usajili mzuri kwa kuboresha kikosi chetu, sasa tunafanya kazi kwa vitendo na si maneno.

"Tumeona msimu huu hatukufanya vizuri, tumeona tatizo la kufanyiwa kazi haraka, tunakutana na mkuu wa benchi la ufundi kwa qjili ya tathmini ya kikosi na mwenendo wa msimu huu na kujadili msimu ujao," alisema Kajula.

## *Yanga mguu mmoja fainali*

INATOKA UKURASA 24

Yanga bao dakika saba baadaye, lakini shuti liliishia tena mikononi mwa kipa Arubi.

Dakika ya 25, timu zote mbili zilifanya mashambulizi, Manaka alipomimina krosi bomba ya juu iliyompita kipa Djigui Diarra, lakini haukuweza kuingia wavuni, wala kuwahiwa na mchezaji yeyote wa Marumo Gallatns na ukaambaambaa nje. Sekunde chache baadaye Yanga walikosa bao.

Mayele aliendelea kukosa mabao, dakika ya 27 alipopiga shuti juu, na dakika ya 31, Moloko alipewa pasi mpenyezo na Mayele, lakini akapiga shuti juu.


# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/05/23 | 17:00 | Aston Villa vs Tottenham Hotspur | 2.18 | 3.40 | 2.95 |
| 02. 13/05/23 | 17:00 | Southampton FC vs Fulham FC | 2.70 | 3.20 | 2.45 |
| 03. 13/05/23 | 17:30 | FC Vizela vs FC Famalicao | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 04. 13/05/23 | 19:15 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 2.65 | 3.15 | 2.24 |
| 05. 13/05/23 | 19:30 | Sunderland AFC vs Luton Town | 2.60 | 3.20 | 2.60 |
| 06. 13/05/23 | 19:30 | Villarreal CF vs Athletic Bilbao | 2.17 | 3.35 | 3.00 |
| 07. 13/05/23 | 19:45 | FC Volendam vs Sparta Rotterdam | 2.85 | 3.45 | 2.24 |
| 08. 13/05/23 | 21:30 | CA Independiente Avellaneda vs CA Tigre | 2.44 | 2.90 | 2.60 |
| 09. 14/05/23 | 00:00 | CA Banfield vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.47 | 2.80 | 2.65 |
| 10. 14/05/23 | 13:30 | Hellas Verona vs Torino FC | 2.29 | 3.05 | 3.10 |
| 11. 14/05/23 | 14:00 | Coventry City vs Middlesbrough FC | 2.70 | 3.25 | 2.42 |
| 12. 14/05/23 | 15:00 | RC Celta de Vigo vs Valencia CF | 2.16 | 3.20 | 3.20 |
| 13. 14/05/23 | 16:30 | VfB Stuttgart vs Bayer Leverkusen | 2.60 | 3.40 | 2.43 |
| 14. 14/05/23 | 17:30 | Rio Ave FC vs Vitoria SC Guimaraes | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 15. 14/05/23 | 18:05 | AS Monaco vs Lille OSC | 2.60 | 3.50 | 2.37 |
| 16. 14/05/23 | 19:00 | Bologna FC vs AS Roma | 3.15 | 3.00 | 2.28 |
| 17. 14/05/23 | 20:00 | Defensa y Justicia vs Estudiantes de La Plata | 2.26 | 2.85 | 2.90 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 11/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 5853 | Bosnia & Herzegovina U19 vs Slovenia U19 | 2.25 | 3.16 | 2.95 |
| 15:00 | 5345 | Mekelakeya vs Saint George FC | 5.08 | 3.73 | 1.57 |
| 15:30 | 2964 | Sioni Bolnisi vs WIT Georgia | 1.79 | 3.52 | 3.88 |
| 15:30 | 3406 | FC Norchi Dinamo Tbilisi vs Kolkheti Poti | 2.31 | 3.44 | 2.66 |
| 15:30 | 4974 | FC Kolkheti Khobi vs FC Spaeri | 2.75 | 3.25 | 2.14 |
| 16:00 | 2165 | Dinamo vs 2 Tbilisi-Gareji | 3.00 | 3.47 | 2.09 |
| 17:00 | 2066 | Arsenal FC Reserve vs Newells Old Boys | 2.21 | 3.17 | 3.01 |
| 17:00 | 5782 | CD Godoy Cruz vs Huracan Reserve | 3.01 | 3.32 | 2.15 |
| 17:00 | 5872 | CA Lanus vs Gimnasia de la Plata Reserve | 1.59 | 3.73 | 4.97 |
| 17:15 | 4826 | AL Khaleej Khor Fakkan vs Al Wasl Dubai | 3.55 | 3.80 | 1.77 |
| 17:15 | 5719 | Jazira Abu Dhabi vs Ittihad Kalba | 1.52 | 4.06 | 4.83 |
| 18:00 | 3024 | Wolkite City FC vs Legetafo Legedadi | 1.62 | 3.43 | 5.20 |
| 19:00 | 1195 | Etehad Alreef vs Al Ittifaq Bhr | 5.59 | 4.14 | 1.47 |
| 19:00 | 2948 | US Ancona 1905 vs Lucchese | 2.00 | 3.09 | 3.50 |
| 19:00 | 3515 | Qalali vs Bouri | 1.62 | 3.79 | 4.57 |
| 19:00 | 3554 | Um Alhassam vs Malkiya Club | 1.95 | 3.27 | 3.53 |
| 19:00 | 4825 | ISA Town vs Najma Manama | 4.67 | 4.05 | 1.57 |
| 19:00 | 5144 | Viimsi JK vs Flora II | 1.57 | 4.37 | 4.91 |
| 19:00 | 5256 | Sonderjyske vs Vejle BK | 2.77 | 3.33 | 2.23 |
| 19:30 | 5358 | Al Nasr Dubai vs Al Sharjah SC | 3.19 | 3.45 | 1.98 |
| 20:00 | 4329 | Hobro vs Fremad Amager | 1.75 | 3.49 | 3.95 |
| 21:00 | 2137 | Renate vs Arzignanochiampo | 2.46 | 2.98 | 2.72 |
| 21:00 | 3892 | America FC SP vs Olimpia SP U20 | 1.30 | 4.96 | 7.65 |
| 21:30 | 1231 | Gubbio vs Recanatese | 1.89 | 3.03 | 4.00 |
| 21:30 | 1717 | AZ Picerno vs Potenza SC | 2.04 | 3.08 | 3.39 |
| 21:30 | 1850 | Celtic W vs Glasgow City W | 2.79 | 3.36 | 2.25 |
| 21:30 | 3129 | Monopoli vs Latina | 2.05 | 2.98 | 3.49 |
| 21:30 | 4665 | Usd Audace Cerignola vs Juve Stabia | 1.98 | 2.99 | 3.71 |
| 21:30 | 5134 | Padova vs US Pergolettese | 1.90 | 2.98 | 4.01 |
| 21:30 | 5849 | Vecomp Verona vs Novara | 2.94 | 2.94 | 2.33 |
| 21:45 | 5766 | Pontedera vs Rimini | 2.45 | 2.77 | 2.93 |
| 22:00 | 2063 | Fiorentina vs FC Basel | 1.37 | 4.75 | 7.07 |
| 22:00 | 3716 | Roma vs Bayer Leverkusen | 2.10 | 3.17 | 3.48 |
| 22:00 | 4630 | Juventus vs Sevilla FC | 1.82 | 3.25 | 4.46 |
| 22:00 | 5126 | West Ham vs AZ Alkmaar | 1.56 | 3.89 | 5.45 |

## IJUMAA - 12/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2285 | KMC vs Singida BS FC | 2.90 | 3.11 | 2.25 |
| 19:00 | 5388 | Slaven Belupo vs Lokomotiva Zagreb | 2.68 | 3.09 | 2.42 |
| 21:00 | 1683 | FC Eindhoven vs Helmond Sport | 1.49 | 4.06 | 5.63 |
| 21:00 | 1856 | Twente vs NEC Nijmegen | 1.45 | 4.40 | 5.80 |
| 21:00 | 3179 | Jong Ajax vs Jong AZ Alkmaar | 2.09 | 3.65 | 2.92 |
| 21:45 | 1852 | Bohemians FC vs Derry City | 2.78 | 3.09 | 2.34 |
| 21:45 | 2786 | Dundalk FC vs Cork City | 1.84 | 3.34 | 3.75 |
| 21:45 | 4317 | St Patricks vs Drogheda Utd | 1.76 | 3.49 | 3.90 |
| 21:45 | 4943 | Galway United vs Wexford Youths | 1.19 | 5.54 | 11.28 |
| 21:45 | 5132 | UCD Dublin vs Shamrock Rovers | 10.27 | 5.55 | 1.20 |
| 21:45 | 5759 | Lazio vs Lecce | 1.66 | 3.46 | 5.01 |
| 22:00 | 4322 | Lens vs Reims | 1.53 | 4.10 | 5.20 |
| 22:00 | 5490 | Mallorca vs Cadiz CF | 2.08 | 2.86 | 3.86 |
| 22:00 | 5722 | Burgos vs Leganes | 2.31 | 2.95 | 3.15 |
| 22:15 | 4722 | Gil Vicente vs Boavista | 2.16 | 3.32 | 3.12 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Alhamisi Mei 11, 2023

Nipashe



Ancelotti akataa bao la De Bruyne UKURASA 22

GUU KWA GUU!...



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Marumo Gallants ya Afrika Kusini, Tshepo Gumede, katika mechi ya nusu fainali mkondo wa kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa wenyeji kushinda 2-0. **NAMPIGAPICHA WETU**

# YANGA SASA MGUU MMOJA FAINALI CAF

## ●●● Morrison, Aziz Ki waiweka pazuri ikihitaji sare yoyote Jumatano kwenda...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, wameingiza mguu mmoja kwenye fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, baada ya jana kuichakaza Marumo Gallatns ya Afrika Kusini mabao 2-0, katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Banjamin Mpaka, Dar es Salaam jana.

**Yalikuwa ni mabao ya wachezaji wa kimataifa kutoka Afrika Magharibi walioamua mechi hiyo, Mburkina Faso Stephane Aziz Ki na Mghana Bernard Morrison, yaliyoifanya Yanga kuwa na kazi ya kwenda kuulinda ushindi huo Jumatano ijayo katika mechi ya mkondo wa pili itakayopigwa Uwanja wa Royal Bafokeng uliopo Rustenberg, Afrika Kusini.**

Inachotakiwa kufanya Yanga kwa sasa kupata ushindi wowote ugenini ama sare yoyote au kufungwa bao moja tu ili kuweka rekodi ya kutinga fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza kwenye historia ya klabu hiyo tangu ilipoanzishwa mwaka 1935.

Aziz Ki alimalizia kazi nzuri iliyofanywa na Tuisila Kisinda dakika ya 63, akitumia mbio zake, aliikimbilia pasi ndefu iliyopigwa kutoka nyuma, akimwacha Ayanda Nkili, halafu akajifanya kama anapiga, lakini haikuwa hivyo, akawazubaisha mabeki wengine na wageni hao, akaiweka kwenye njia.

Mburkina Faso huyo alikuwa anakimbilia golini kwa kasi akaikuta kwenye njia na kupita shuti upande wa kulia mwa kipa Washington Arubi ambaye alikuwa kwenye kiwango bora jana kwa kuokoa michomo mingi, lakini alijikuta akisimama tu na kuuangalia mpira huo ukijaa wavuni.

Wawakilishi hao wa Tanzania walijihakikishia ushindi walipopata bao la pili kwenye dakika nne za nyongeza likifungwa na mtokea benchini, Bernard Morrison.

Alikuwa ni Fiston Mayele aliyeondoka na mpira kwa umbali mrefu, akitumia makosa ya mabeki wa Marumo Gallants kupanda mbele kutaka kuwasaidia washambuliaji wao kurudisha bao, akammegea pande Morrison aliyebaki yeye na kipa Arubi na beki mmoja.

Alichofanya ni kuwahadaa, akawaruka, akaanguka, akanyanyuka na kuuwahi mpira, kabla ya kuujaza wavuni, akiwanyanyua mashabiki waliojitokeza kwa wingi uwanjani hapo jana.

Wageni hao watawala mechi kwa vipindi vyote viwili na Yanga ililazimika kuwatoa Aziz Ki, baada ya kufunga bao, Jesus Moloko na Yannick Bangala, wakiwaingiza Morrison aliyekwenda kufunga bao la pili, Clement Mzize na Mudathir Yahaya.

Mechi ilianza kwa timu zote kuamua kucheza kati zaidi, huku Marumo Gallants ikionekana kuwa na viungo wazuri wa kuuchezea mpira na walitumia ufundi wao kupozesha, Yanga nayo ikaingia kwenye mfumo huo.

Dakika ya saba Edgar Manaka alimtoka Kibwana Shomari kwenye wingi ya kulia na kupiga krosi ambayo ilitoka nje kidogo ya lango.

Kisinda alifanya kazi ya ziada dakika ya 13, alipowahadaa mabeki wa Marumo Gallants na kuubetua mpira juu langoni mwa wapinzani wao, lakini wachezaji wa Yanga wakachelewa.

Mayele, dakika ya 14, aliambaa na mpira mbele akawadanganya mabeki, akageuka ghafla na kupiga shuti lililodakwa na kipa Arubi, ukamtoka, akanyanyuka na kuukimbilia tena kabla haujatoka kona.

Mayele tena, nusura aipatie

INAENDELEA UKURASA 23

## Simba njia nyeupe kwa Yahya Mbegu

**Na Saada Akida**

WAKATI Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Iman Kajula, akiweka wazi kuwa wamejipanga vizuri kuhakikisha wanafanya maboresho makubwa ndani ya kikosi cha timu hiyo kuelekea michuano ya Africa Super League itakayoshirikisha timu kubwa nane barani humu, milango tayari ipo wazi kumnasa beki wa kushoto wa Ihefu FC, Yahya Mbegu.

Simba ni klabu pekee kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki, itakayoshiriki michuano hiyo mikubwa Afrika ambayo inatarajiwa kuanza Oktoba mwaka huu.

Na kuelekea msimu mpya, Simba imekuwa ikihusishwa na usajili wa Mbegu, ambaye amekuwa katika kiwango bora zaidi msimu huu akiwa na kikosi cha Ihefu FC, na sasa mkataba wake unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu na bado hajaanza mazungumzo ya kuongeza kandarasi nyingine na timu yake hiyo.

Taarifa zilizolifikia gazeti hili ni kwamba nyota huyo tayari ameingia katika rada za Simba na yupo katika rada za viongozi wa Simba kwa ajili ya kuinasa huduma yake kwa msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Ihefu FC, Zagalu Chalamila, alisema hawana taarifa au ofa kutoka Klabu ya Simba kuhitaji huduma ya Mbegu ambaye mkataba wake unafikia ukingoni baada ya ligi kumalizika.

Alisema nyota huyo yuko katika mipango ya benchi lao la ufundi akiwa miongoni mwa wachezaji ambao wamependekezwa na kocha kusalia ndani ya kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao.

"Mbegu mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, bado hatujaanza kufanya mazungumzo na beki huyo, hatuna haraka naye, kama itatokea timu inamhitaji yeye ndiye ataangalia," alisema Chalamila.

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042